# Nipashe

Alhamisi Desemba 17, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580432

www.ippmedia.com

MWANGA WA

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**Kijana** afungwa jela maisha kwa kumbaka mtoto wa miaka 3

UKURASA 5



RIPOTI MAALUM

**Soko** la ndizi laporomoka Kagera, Kaskazini

UKURASA 4

**Depay aikataa Barca, PSG**

UK.20

# Waziri Mpango awasha moto



• **Aagiza** maofisa 22 TRA kusimamishwa, kuchunguzwa, wamo mameneja wa mikoa... *Endelea ukurasa 2*

## KUMRADHI



KATIKA gazeti la Nipashe toleo la jana, kulikuwa na picha ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ikimwelezea kuwa ni Meja Jenerali Julius Mbung'o.

Usahihi ni kwamba cheo chake ni Brigedia Jenerali na jina lake ni John Mbung'o. Tunaomba radhi kwa makosa yaliyojitokeza. – **MHARIRI**.

## Utendaji mawaziri wamkosha Magufuli

UKURASA 2



Rais Dk. John Magufuli, akimkabidhi nyenzo za kazi Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, baada ya kuapishwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jijini Dodoma. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store




## DC awacharaza viboko wanafunzi, w/biashara

UKURASA 3


**MICHEZO** KAZE ATAMBA KIKOSI KIMEIVA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Utendaji mawaziri wamkosha JPM

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli jana, aliongoza kikao cha kwanza cha Baraza la Mawaziri na kueleza kufurahishwa na kazi nzuri zinazofanywa na watendaji hao.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika Ikulu ya Chamwino, Dodoma, ambacho ni cha kwanza tangu kuanza kwa awamu ya pili ya miaka mitano, Rais Magufuli alisema amekiitisha ili kujua mwelekeo.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi na baadhi ya mawaziri walihudhuria kwa mara ya kwanza tangu kuteuliwa kwao.

Baada ya Rais Magufuli kuingia katika kikao hicho, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, alitoa maelezo ya awali kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, anatakiwa kuapa na kuwa mjumbe wa Baraza la Mawaziri.

Dk. Mwinyi alikula kiapo mbele ya Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, na tukio hilo ni kwa mujibu wa taratibu za baraza la mawaziri zinazomtaka kufanya hivyo kabla ya kushiriki.

Akizungumza katika kikao hicho, Rais Magufuli alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuwa mjumbe wa baraza hilo.

"Mheshimiwa Mwinyi karibu sana kwenye kikao chetu, waheshimiwa wajumbe karibuni sana na hongereni kwa kuwa wajumbe wa Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa karibuni, leo tumekutana wote ili tujue mwelekeo lakini kwa ujumla mmeanza vizuri sana, hongereni sana."

**MAWAZIRI 23**

Mawaziri waliohudhuria kwa mara ya kwanza ni Dk. Damas Ndumbaro (Maliasili na Utalii), Mashimba Ndaki (Mifugo na Uvuvi), Prof. Adolf Mkenda (Kilimo), Dk. Leonard Chamuriho (Ujenzi na Uchukuzi). Elias Kwandikwa (Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa) na Juma Aweso (Maji).

Wengine ni Dk. Dorothy Gwajima (Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), Prof. Kitila Mkumbo (Ofisi ya Rais-Uwekezaji), Geoffrey Mwambe (Viwanda na Biashara) na Dk. Faustine Ndugulile (Mawasiliano na Teknolojia ya Habari).

**WA ZAMANI**

Mawaziri wa zamani waliohudhuria ni Kapteni George Mkuchika (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), William Lukuvi (Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi) Innocent Bashungwa (Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo), Jenista Mhagama (Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu) na Ummy Mwalimu (Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano).

Wengine ni Dk. Mwigulu Nchemba (Katiba na Sheria), Dk. Philip Mpango (Fedha na Mipango), Prof. Joyce Ndalichako (Elimu, Sayansi na Teknolojia), George Simbachawene (Mambo na Ndani ya Nchi), Prof. Palamagamba Kabudi (Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki), Selemani Jafo (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Dk. Merdard Kalemani (Nishati), Doto Biteko (Madini).



Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma na Mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. David Mwamfupe, akizungumza jana, alipokuwa akitoa mada kwenye kongamano la wahitimu wa mahafali ya 11 ya chuo hicho, chuoni hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Mpango aiwashia moto TRA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amemwagiza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, kuwasimamisha kazi watumishi 22 wa mamlaka hiyo.

Miongoni mwa watumishi hao ni mameneja wa mikoa wa TRA na kwamba wanatuhumiwa kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo ikiwamo kujihusisha na ufisadi na uzembe kazini, hivyo kuikosesha serikali mapato.

Dk. Mpango alitoa maagizo hayo jijini Dodoma jana, katika kikao kazi, alipokutana na Bodi ya Wakurugenzi, menejimenti na mameneja wa mikoa wa mamlaka hiyo kupanga mikakati namna ya kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya kodi na maduhuli ya serikali.

Aliagiza uchunguzi wa kina ufanyike kwa watumishi hao wanaotuhumiwa na vitendo vya rushwa, kutosimamia ipasavyo matumizi ya mashine za kutolea stakabadhi (EFD), kuwabambikia kodi kubwa wafanyabiashara na kuagiza apatiwe taarifa ya utekelezaji wa maelekezo hayo ndani ya siku 90 kuanzia jana.

Watumishi hao ambao aliagiza wasimamishwe kazi ni Brighton Kasilo, ofisa wa TRA Tanga; Kaimu Meneja wa Nkasi, Rogers Mkama, Meneja wa Ukaguzi Shinyanga, Sara Senso, na Meneja wa EFD Kwibin Nyamuhanga.

Wengine ni Meneja wa Mkoa Kabula Mwemezi; Meneja wa Mkoa wa Kigoma, Jacob Mtemang'ombe, Meneja wa TRAc Kasulu, Benward Mwakatundu na maofisa wa mkoa wa Songwe, Janeth Mlack, na Joshua Samwel.

Pia wamo Msimamizi wa Kituo cha Tarakea, Maududi Tingwa, na maofisa wa Same, Adam Benta na Adam Ruhusa; Hilda Mahenge, Ibrahim Lyndama na Geofrey Mwinuka wa Njombe.

Watumishi wengine ni Meneja wa Biharamulo, Alex Chacha, maofisa mkoa wa Ilala, Stephen Kauzeni, Kimweli, Ngobya, Raphael Meng'alai, Benedict Kasele na Nicodemus Mwandago, na Kaimu Meneja wa Ruangwa, Florian Rubambwa.

"Nakuagiza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Dk. Edwin Mhede, uwapumzishe kazi kuanzia leo (jana) kwa mujibu wa kanuni ya 37 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003 na umwagize Mkuu wa Idara ya Mambo ya Ndani awachunguze wahusika wote ndani ya siku 90 na nipatiwe nakala ya taarifa ya uchunguzi na hatua zilizochukuliwa dhidi ya kila mmoja," alisema.

Dk. Mpango pia alimwagiza Dk. Mhede, kufanya uhamisho wa lazima wa maofisa waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi na kwamba anatambua kazi hiyo itagharimu fedha nyingi, lakini ni bora kufanya hivyo. Alisema kukaa kwao muda mrefu kwenye vituo vyao kunaathiri utendaji kwa kuwa wengi wao wana mitandao ya kuiba fedha za umma. Pia aliiagiza TRA kusimamia kikamilifu matumizi ya EFD nchini kote na kubaini stakabadhi za kughushi na mashine bandia zinazotumiwa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu na pia kutoa muda wa siku 15 kuanzia sasa hadi Desemba 31, kuhakikisha changamoto ya kufutikafutika kwa stakabadhi zinazotolewa na EFD inapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

"Ili kuweka kumbukumbu ni lazima utoe nakala ya risiti kwani usipofanya hivyo baada ya siku chache inafutika. Jamani kwa nini iwe risiti za TRA tu? Mbona kwenye Supermarkets wao hazifutiki! Mlishanieleza kuwa sasa mmeanza kusambaza karatasi za risiti ambazo hazifutiki, lakini kiuhalisia bado! Hatuwezi kuendelea na utaratibu huo bila kufikia mwisho wake," alionya.

Eneo lingine alilotilia mkazo Dk. Mpango ni hatua ya baadhi ya watumishi wa TRA wasio waaminifu wanaowabambikia wafanyabiashara kodi kubwa na kuzishikilia akaunti zao za benki na baadaye kuwadai rushwa, ili wawapunguzie kodi jambo alilosema linawakwaza wafanyabiashara na kuikosesha serikali mapato.

"Baadhi ya wafanyabiashara hasa wadogo wameanza kukwepa kufanya miamala kupitia benki na kuweka fedha za mauzo benki kwa sababu taarifa za benki zinatumiwa na TRA kufanya makadirio ya juu mno ya kodi kwa kuangalia ukubwa wa miamala ambayo kwa sehemu kubwa ni fedha za wafanyabiashara wakubwa waliowakopesha bidhaa wafanyabiashara hao.

Ninaiagiza Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato ikalichunguze eneo hilo, ili ukadiriaji wa mapato uwe wa haki na makadirio hayo yaakisi ukubwa wa biashara," alisisitiza Dk. Mpango.

Kuhusu zawadi kwa watoa taarifa za wakwepa kodi, Dk. Mpango alieleza kuwa kuna malalamiko ya watoa taarifa kutolipwa zawadi zao, huku baadhi ya watumishi wa TRA wasio waaminifu wakitoa taarifa zao kwa wakwepa kodi hali ambayo ni hatari kwa usalama na maisha yao na kuutaka uongozi wa TRA kumwandalia taarifa ya mwaka mmoja ya namna walivyowapa zawadi watoa taarifa hao ambao ni muhimu kwa kuwa wanaokoa fedha za serikali.

Alipiga marufuku TRA kufunga biashara za wafanyabiashara kwa kushindwa kulipa kodi badala yake watumie njia ya kukaa nao na kujadiliana namna ya kulipa kodi hizo na kwamba uamuzi wa kufunga biashara uwe wa mwisho baada ya njia zote kushindikana na mwenye mamlaka ya mwisho ya kufanya hivyo ni Kamishna Mkuu wa TRA.

Maeneo mengine aliyoyagusia na kutoa maelekezo ya kuboresha ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa kodi ya majengo, kudhibiti ukwepaji wa kodi kwenye biashara ya vyuma chakavu, kuongeza ukusanyaji wa kodi katika sekta ya madini, kubadilisha nyaraka kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili, kurejesha imani ya wafanyabiashara kwa TRA na kumwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, kuanzisha ofisi itakayoshughulikia malalamiko ya kodi kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

## HABARI KITAIFA

# DC acharaza viboko wanafunzi, w/biashara vyuma chakavu



**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi (pichani) amewacharaza viboko wanafunzi na wafanyabiashara wa vyuma chakavu waliobainika kununua viti vya Shule ya Sekondari Sinoni, jijini hapa.

Akitoa adhabu hiyo jana, katika Shule ya Sinoni kwa vijana watano waliohusika kununua viti hivyo, Kihongosi alisema serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kuhakikisha watoto wanapata elimu, lakini anasikitishwa kuona wafanyabiashara wakinunua miundombinu iliyopo kwenye matumizi.

"Serikali inatoa fedha nyingi kuhakikisha elimu inaendelezwa ili taifa liondokane na ujinga, leo mnanunua kiti Sh. 500, wakati kiti hicho kinatengenezwa kwa gharama ya Sh. 100,000, huu ni ujinga hamfikirii thamani ya miundombinu inayotolewa na serikali?" Alihoji.

Alimwagiza mkuu wa shule hiyo, kuhakikisha watoto walioiba viti wanasimamishwa masomo hadi wazazi watakapolipa viti hivyo, pamoja na wafanyabiashara hao kupelekwa mahabusu hadi watakaposema viti hivyo vinalipwaje.

Alimwagiza pia mwalimu huyo kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa vifaa vya shule kujua idadi ya vilivyoharibika, kupotea na vinavyoendelea kutumika lengo likiwa ni kujua hali halisi ya miundombinu ya shule.

Pia, aliongea na baadhi ya wananchi wa Kata ya Sinoni, kuwajibika katika elimu za watoto wao ikiwa ni pamoja na kusimamia vyema watoto kuhudhuria shuleni badala ya kuhangaika mtaani kutafuta vyuma chakavu na kujihusisha na biashara jambo linalosababisha kuwa na tamaa ya kuharibu miundombinu ya serikali.

Wazazi wa wanafunzi waliokamatwa walikiri kuwa watoto wao wapo nyumbani baada ya kusimamishwa na uongozi wa shule hadi kikao cha bodi kitakapofanyika kwa ajili ya uamuzi wao.

"Sisi tumelipokea kwa masikitiko jambo hili la watoto wetu kuhusishwa na wizi wa viti kwa kuwa tunajitahidi kuhakikisha wanasoma, ili watuletee maendeleo baadaye wakati mwingine tunalala hadi njaa kwa ajili ya kutoa mahitaji yao, lakini matokeo yake wanajiingiza kwenye makundi yasiyofaa," alisema Saruni Laizer, mmoja wa wazazi wa watoto waliokamatwa na wizi wa viti vya shule.

Vile vile, Mkuu huyo Nteles Lorna, alisema walibaini upotevu wa viti 108 baada ya mitihani ya kidato cha nne kufanyika kutokana na viti hivyo kupungua na kwamba uchunguzi wa kubaini viti hivyo ulianza na kugundulika baadhi ya wanafunzi kuhusika na wizi huo.

"Tulianza kuweka mitego hadi kwa walinzi na juzi ilipokuwa Sikukuu ya Uhuru, mlinzi aliona watoto hao wakirusha viti juu ya ukuta na kuvichukulia nje ya ukuta na kuvipeleka kwa wauzaji wa vyuma chakavu," alisema Lorna.

Operesheni ya kuhakiki miundombinu ya shule hiyo ilifanywa na Ofisa Tarafa ya Elerai, mkoani hapa, Titho Cholobi na baada ya kubaini upotevu huo alimshirikisha Mkuu wa Wilaya.

"Nilipata taarifa kwa wasamaria wema na nilifika kuona hali ilivyo, tulifanikiwa kuwatembelea wanunuzi waliohusika kwa bahati nzuri wamekamatwa, lakini tukawakamata na watoto wanane wanaohusishwa na jambo hili," alisema Cholobi.

Cholobi alisema kiti kimoja thamani yake ni Sh. 100,000, lakini bila aibu wanunuzi wananunua kwa Sh. 500, kama chuma chakavu jambo ambalo ni la kuhujumu miundombinu ya serikali.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Sinoni Michael Kivuyo, alisema kata hiyo ina idadi kubwa ya wauzaji wa vyuma chakavu pamoja na watoto wanaoacha kwa makusudi kwenda shuleni na kujiingiza katika biashara hiyo.

# Waagizwa kasi ya ukusanyaji mapato

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, wameagizwa kusimamia ukusanyaji mapato, ili serikali ipate fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alitoa agizo hilo juzi wakati wa kuapishwa madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Alisema madiwani wana jukumu la kwenda kusimamia ukusanyaji mapato, ili serikali ipate fedha ambazo zitatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa.

"Mnapokuwa kwenye usimamizi wa ukusanyaji mapato, hakuna kumfumbia mtu macho kwa sababu serikali ambayo haikusanyi mapato haiwezi kusonga mbele," alisema Mboneko.

Pia aliwataka madiwani hao wakasimamie fedha za miradi ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwenye maeneo yao, ili ijengwe kwa kiwango kinachotakiwa pamoja na kuibua miradi mipya.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, aliwataka madiwani hao, wakafanye kazi ya kuwatumikia wananchi na si kutanguliza maslahi yao binafsi.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, aliahidi ataisimamia vizuri halmashauri kwa kushirikiana pia na madiwani, ili kuhakikisha mji wa Shinyanga una kuwa kimaendeleo.

# Nipashe yatunukiwa cheti kuripoti uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu**

GAZETI la Nipashe limetunukiwa cheti na Asasi ya Sauti ya Mama Africa Foundation (SAMAFO), kwa kuhabarisha umma kuhusu elimu ya mpigakura na ushiriki wa upigaji kura.

SAMAFO imetambua mchango wa Nipashe katika kuripoti taarifa mbalimbali kuhusu uchaguzi kuanzia kipindi cha kampeni hadi siku ya uchaguzi mkuu wa Oktoba, 28, mwaka huu.

Vyombo vilivyotunukiwa vyeti ni vituo vya redio 13 za jijini Mbeya na Nipashe upande wa magazeti. Akitoa vyeti hivyo kwa niaba ya asasi hiyo, mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alivipongeza vyombo vya habari, ikiwamo gazeti hili kwa kutoa habari kuhusu uchaguzi wa mwaka huu.

"Tunaipongeza sauti SAMAFO kwa kutambua mchango wa vyombo vya habari na kuwapa zawadi ya vyeti, uchaguzi ulikuwa wa amani na utulivu," alisema Ntinik na kuongeza...

"Tasnia ya habari ina nafasi kubwa katika kutoa taarifa hata kipindi cha corona tulitegemea taarifa kutoka kwao, hatimaye tukaishinda corona kwa kumwomba Mungu, mwaka huu ni kipekee."

Ntinika alisema pia yeye binafsi anavipongeza vyombo vya habari katika mkoa wa Mbeya, vilivyoshiriki katika uchaguzi kwa kutoa matokeo na hatimaye, kutangazwa Rais John Magufuli kuwa mshindi wa kiti cha urais.

Mkurugenzi Mtendaji wa SAMAFO, Tabitha Bugali, alisema waliona ni vyema kuongeza nguvu ya kuelimisha umma kupitia vyombo vya habari, ikiwamo gazeti pamoja na redio 13 za jijini humo.

"Gazeti la Nipashe kupitia mwandishi wao Christina Mwakangale aliandika habari kwetu juu ya elimu ya mpigakura na kuzitoa kwenye gazeti, hususan kutoa ushawishi wanawake kupigakura na walemavu kupewa kipaumbele," alisema Bugali. "Tumeona tuseme asante na kutoa shukrani zetu hizi kwa kupitia cheti hiki kiwe kumbukumbu na alama ya shukrani zetu kwao, naomba wapokee na kutukubali," alisema Bugali.

Pia, aliongeza kwa kuishukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Wakurugenzi wa Halmashauri za Mbeya Jiji na Mbeya DC, watendaji wa kata, mitaa, vitongoji, wenyeviti na wananchi walioitikia mikutano ya uelimishaji.

Alisema elimu kwa wapigakura, ilisaidia kuwapa mwanga na uhuru wa kuchagua kile wanachoona kinafaa.

Bugali alisema asasi hiyo iliyafikia makundi maalumu katika jamii, ikiwamo yote ya wanawake, watu wenye ulemavu, vijana na wazee katika maeneo tofauti ya jijini Mbeya, wakati wa kampeni.


## Lawyers Environmental Action Team

### Publication of Bi annual Income and Expenditure.

Lawyers Environmental Action Team is, local Non-Governmental Organization which was found in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with (Certificate of Compliance No. 1985).

**Vision:** Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.

**Mission:** To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, the Lawyers Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expenditure from January 2020 to June 2020.

**Bi-Annual income and Expenditure for the period from January to June 2020**

| | |
|---|---|
| **Income:** | |
| Receipt from Donors | 625,152,008.13 |
| Bank Interest | 113,008.00 |
| **Total Income** | **625,265,016.13** |
| **Expenditure:** | |
| Legally empower Urbanites living in Dar es Salaam to access and enforce a right to live in clean environment | 76,051,612.25 |
| Examining the Extractive Legal regime in Tanzania | 34,985,252.00 |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili in Tanzania | 235,270,334.71 |
| Environmental Advocacy SJRS in Rukwa Tanzania | 256,238,774.05 |
| Human & Admin Resources Activities | 22,719,043.12 |
| **Total Expenditure** | **625,265,016.13** |
| **Surplus/Deficit:** | - |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Legal Services Facility (LSF), Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania) and the International Union for Conservation of Nature –Netherlands (IUCN-NL).

**Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),**
**Mazingra Street, MikochenìB, House No 8,**
**P.O. Box 12605, Dar es Salaam;**
**Email: info @leat.or.tz.**

RIPOTI MAALUM

# Soko la ndizi laporomoka

## ■Kagera, Kaskazini walia, Mbeya kicheko

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wakulima wa ndizi nchini, wamelalamika kuporomoka kwa soko la bidhaa zao kiasi cha kulazimika kuuza kwa bei ya hasara na wengine kutupa bidhaa zao zinapooza.

Uchunguzi wa Nipashe katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Kagera na Mbeya, umebaini bei ya zao hilo imeporomoka na baadhi ya wakulima wanalazimika kuuza mkungu wa ndizi kwa Sh. 500.

Nipashe ilipomtafuta Waziri wa Kilimo, Profesa Adoph Mkenda, kuzungumzia suala hilo, alisema kwa sasa msisitizo wameuweka katika uwekezaji na biashara kuhakikisha mazao yanayozalishwa nchini yanaongezwa thamani.

Alisema uongezwaji wa thamani katika mazao yote utasaidia kumwongezea mkulima kipato na kuleta unafuu wa maisha kiuchumi.

"Kwa sasa serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi kujiunga katika ushirika ili wawe na sauti moja na kutafuta masoko kwa pamoja ikiwa bidhaa hizo zitaongezwa thamani," alisema.

Gladness Kiungai, mfanyabiashara wa ndizi katika Soko la Tengeru, alisema kwa miaka miwili sasa bei ya ndizi imeshuka ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Alikumbusha kuwa mwaka 2018, mkungu mkubwa wa ndizi wenye vichani 10 walikuwa wakiuuza kati ya Sh. 50,000 na 70,000 lakini kwa sasa wanauuza kwa Sh. 20,000 hadi Sh. 25,000.

"Mwaka 2018, kati ya Oktoba hadi Desemba ndizi zilikuwa zinauzwa kwa bei ya Sh. 50,000 hadi 70,000, lakini kuanzia mwaka 2019, bei imeshuka sana," alilalamika Gladness.

Alisema kufungwa kwa mipaka kutokana na ugonjwa wa Covid-19 na kutokuwapo kwa soko la uhakika la kuuzia bidhaa hiyo, kumechangia kushuka kwa bei ya ndizi.

"Mipaka ilipofungwa kutokana na ugonjwa wa corona, wanunuzi walisitisha kununua ndizi. Pia, kufungwa kwa baadhi ya hoteli kubwa za kitalii katika Mkoa wa Arusha kuliathiri na kusababisha bei ya ndizi kushuka kwa kasi," Gladness alibainisha.

Mfanyabiashara mwingine wa ndizi jijini Arusha, Beatrice Nanyaro, alitaja sababu nyingine ya kuporomoka kwa bei ya ndizi kuwa ni kushuka thamani kutokana na ongezeko la wakulima wa zao hilo ilhali hakuna wanunuzi.

"Mwaka huu wa 2020, ndizi zimeshuka kabisa, ukienda sokoni unanunua kwa Sh. 1,500 hadi 3,000 mkungu wa ndizi ambao awali ulikuwa ukiuzwa kiasi cha Sh.10,000.

"Ugonjwa wa corona na kukosekana kwa soko la nje la uhakika kumeathiri sana kilimo cha ndizi, kimekuwa kilio kikubwa kwa wakulima, tunaiomba serikali yetu itusaidie kutafuta soko la uhakika



kwa kuwa biashara hii ndiyo inatuingizia kipato cha kulisha familia na kusomesha watoto wetu," alisema .

Mary Kiungai na Sifaeli Akyo, wakulimaa wa ndizi katika Kitongoji cha Stoni, Kata ya Sing'isi, walisema kilimo cha ndizi kilikuwa kikiwanufaisha awali kwa kuwa waliuza ndizi kwa bei ghali.

"Miaka ya nyuma mwezi kama huu (Desemba) tulikuwa tunawauzia wafanyabiashara ndizi kwa gharama ya juu, lakini mwaka huu tena mwezi Desemba tunaotegemega bei kupanda, imekuwa tofauti kabisa, ndizi zimekuwa bwerere.

"Kwa sasa kilimo cha ndizi kimekuwa hasara kwa wakulima kwa kwa tunauza ndizi mkungu Sh. 500 mpaka 1,000 kwa kuwa wafanyabiashara nao wanasema hakuna wanunuzi," Akyo alilalama.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa ndizi katika Soko la Tengeru, Angness Kitomari, alisema kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo, kumesababishwa na kuyumba kwa uchumi kutokna na mlipuko wa virusi vya corona na ongezeko la wakulima wa zao hilo. Alisema awali kulikuwa na wasafirishaji wa bidhaa hiyo waliyoipeleka Kenya kupitia Mpaka wa Namanga lakini kutokana na corona, mipaka ilifungwa, hivyo wanunuzi hao hawaendi tena kwenye masoko kununua zao hilo.

**VIWANDA VIDOGO**

Mkoani Kilimanjaro, wakulima wa ndizi wanaiomba serikali kuwasaidia mashine zitakazowasaidia kuanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani zao hilo.

Wamesema kwa sasa mkungu mmoja wanauuza shambani kwa Sh. 2,500 kutoka Sh. 10,000 walivyouza awali na wakati mwingine hali inakuwa mbaya zaidi na kulazimika kuuza mkungu kwa Sh. 500.

Katika Soko la Mwika wilayani Moshi, mkulima Neema Urio, aliambia Nipashe juzi kuwa walikuwa wakiuza mkungu mmoja kwa Sh. 10,000 kwa ndizi za vichane sita na Sh. 25,000 kwa ndizi za vichane 15.

"Kwa sasa hakuna soko kabisa, ndizi ya vichane vitatu inauzwa kwa Sh. 500 na ya vichane 15 inauzwa kwa Sh. 3,000 hadi 5,000, tunaiomba serikali kuangalia namna ya kuwasaidia wakulima ili kujikimu kiuchumi," alisema.

Zawadi Uwiso, mkulima wa Uru Mawela, alisema zipo baadhi ya aina ya ndizi hazina soko kabisa, hivyo wakulima kulazimika kuziacha ziozee shambani.

"Hii inasababisha mkulima kutonufaika na zao hilo kwani kwa sasa imepelekea hadi pombe ya mbege kushuka kutoka Sh. 15,000 kwa ujazo wa lita 20 hadi kufikia Sh. 6,500," alibainisha.

Delisia Masawe, mkazi wa Kata ya Kisale wilayani Rombo, alisema soko hilo kushuka ni kutokana na mipaka ya nchi za jirani kufungwa tangu kulipuka kwa ugonjwa wa Covid-19. Alisema mkungu uliokuwa unauzwa Sh. 25,000 kwa sasa unauzwa Sh. 3,000 hadi 5,000.

"Kwa sasa ndizi zinaiva shambani, hatuna sehemu ya kupeleka, hata tukipeleka sokoni bado gharama ni kubwa sana hasa katika kusafirisha, nako ukifika hakuna masoko.

"Kipindi cha nyuma, tulikuwa na uwezo wa kusafirisha ndizi hadi Dar es Salaam kwa ajili ya kusafirisha nje, lakini kwa sasa wafanyabiashara hao wamekuwa wakichukua kiasi kidogo cha kutosheleza Dar na mikoa jirani," alisema.

Teddy Felix, mfanyabiasha wa ndizi katika Kijiji cha Uru Kitandu, alisema awali walikuwa wanapakia gari aina ya fuso 10 hadi 12 kwa siku lakini sasa zinapita hadi siku mbili bila kupata kazi ya kupakia ndizi.

Mkurugenzi wa Wilaya ya Rombo, Godwine Chacha, alisema kwa sasa kumekuwa na ongezeko la ndizi na kudorora kwa bei ya zao hilo kutokana na mipaka kufungwa.

Alisema kuwa katika kuhakikisha wanatatua tatizo hilo, Wizara ya Kilimo imeichagua Rombo kuwa miongoni mwa wilaya 30 ambazo zinatarajiwa kuboresha sekta ya kilimo na mifugo.

Alisema miongoni mwa mazao waliyoyandikwa kuingia kwenye mradi ni parachichi, ndizi na kahawa.

"Ndizi nyingi kutoka za Rombo zinauzwa nchi jirani ya Kenya lakini kufuatia mlipuko wa Covid-19, Watanzania wengi wamekuwa na hofu ya kupeleka ndizi huko.

"Tumefanya jitihada mbalimbali za kuhakikisha tunawasaidia wakulima wetu ikiwa ni pamoja na kushirikisha mashirika yasiyo ya kiserikali kuwekeza katika uongezaji wa thamani.

"Pia, kuna taasisi binafsi ambayo kwa sasa ipo wilayani Rombo inawaelimisha wakulima namna bora ya kuacha tabia ya kuuzia mazao ya ndizi yakiwa shambani na badala yake kukusanya na kutafutafa soko la pamoja katika mikoa mbalimbali ndani ya nchi," alisema.

Simoni Msoka, Ofisa Kilimo Mkoa wa Kilimanjaro, alisema ndizi mkoani huko zimeongezeka kwa kiwango kikubwa kutokana na mvua nyingi zilizonyesha, hivyo kuwa nafuu kwa mlaji na tatizo kwa mkulima.

Alisema jitihada za makusudi zinaendelea katika kuhakikisha wanapatikana wawekezaji watakaosaidia kuongeza thamani kwa bidhaa hizo ili kuleta tija kwa mkulima.

Mkoani Kagera, baadhi ya wakulima wa zao hilo wamelalamikia kukosekana kwa soko, hivyo kuendesha kilio kwa hasara.

Ruga Chiiza, mkulima wa zao hilo kutoka Kata ya Kitwe wilayani Kyerwa, alisema soko limeshuka na kuna haja serikali kuandaa mkakati kuwanusuru wakulima.

Chiiza alisema amefanya kazi hiyo kwa zaidi ya miaka 20 na kwamba kumekuwa na mabadiliko ya bei kupanda mara kwa mara lakini mwaka huu wanashuhudia kushuka zaidi. Alisema ndizi shambani inauzwa kwa Sh. 1,500 hadi 4,000 kwa mkungu kutegemea na ukubwa na ubora wa bidhaa.

"Maandalizi yanategemea eneo la ukubwa wa ardhi, mimi nina ekari mbili, kwa mwezi ninavuna mikungu zaidi ya 30 au kwa wiki 12, ukiangalia gharama nimetumia Sh. milioni moja, mbolea gari ndogo Sh. 25,000 na kubwa ni Sh. 50,000. Hii bei ya sasa ni hasara tupu," alilalamika.

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Kagera, Baraka Rwise, alikiri uzalishaji wa zao umekuwa mwingi, lakini tatizo liko kwenye upatikanaji wa soko.

Alibainisha kuwa Mkoa wa Kagera unazalisha ndizi takribani tani milioni 2.4 kwa mwaka lakini ni nusu tu inayouzwa na kutumika na kiasi kingine kinaharibika.

**MBEYA HALI TOFAUTI**

Wakati hali ya soko ikiwa mbaya kwa mikoa ya Kagera, Arusha na KIlimanjaro, mkoani Mbeya bei ya ndizi imepanda kutoka wastani wa Sh. 8,000 hadi 13,000 kwa mkungu mmoja ndani ya kipindi cha miezi miwili kuanzia mwezi Novemba katika baadhi ya masoko ya Jiji la Mbeya.

Kupaa kwa bei ya bidhaa hizo kunadaiwa kusababishwa na hali ya hewa katika kipindi hiki cha baridi wilayani Rungwe, mahali ambako ndizi hizo zinalimwa kwa wingi kulinganishwa na maeneo mengine ya mkoa huo.

Wafanyabiashara wa soko la Uyole wanasema katika kipindi hiki cha baridi wilayani Rungwe, ndizi huchelewa kukomaa na hivyo kusababisha uhaba wa zao hilo sokoni.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Salome Medson, alisema pamoja na kwamba ndizi hizo zimepanda sokoni na hata kwa wakulima.

"Ndizi zinapokuwa chache sokoni, bei inaongezeka kwa sababu kiwango cha ndizi kinachopatikana huwa hakitoshelezi mahitaji ya wateja na hivyo tunalazimika kuongeza bei," alisema Salome.

Mfanyabiashara wa ndizi katika Soko la Kiwira wilayani Rungwe, Sifa Mwanjejele, aliliambia Nipashe kuwa ndizi aina ya jamaika wananunua shambani kati ya Sh. 2,500 na 3,000 kwa mkungu na kuziuza kwa bei ya kati ya Sh. 3,500 na 4,000. Alisema ndizi aina ya matoki zinauzwa kati ya Sh. 6,000 na 7,000 kwa mkungu na kwamba bei hizo kwa sasa zimepanda kutokana na hali ya upatikanaji kuwa ngumu kipindi hiki.

"Hizi ndizi zikifika kwenye Soko la Kiwira, tunawauzia wateja wa Malawi kuanzia Sh. 10,000 na kuendelea lakini kwa miezi ya nyuma hasa mwezi Oktoba, hakuna ndizi ambayo ilikuwa inauzwa kwa bei ya zaidi ya Sh. 8,000," alisema Sifa.

Mwaka 2017 Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani mkoani Mbeya, aliwaagiza viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kuweka mfumo mzuri wa uuzaji wa zao hilo ili wakulima wanufaike badala ya mataifa jirani ikiwamo Malawi, Zambia na Afrika Kusini kunufaika.

**Imeandikwa na Nebart Msokwa, Mbeya. Mary Mosha, Moshi. Allan Isack, Arusha na Restuta Damia, Bukoba**

HABARI KITAIFA

# Jela maisha kwa kumbaka mtoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi, imemhukumu Ally Kacha (27) mkazi wa Kijiji cha Simana, Mtama, kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto wa umri wa miaka mitatu.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa bila shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka. Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa kwa nini asipewe adhabu kali kwa kosa lililokuwa mbele yake na kujitetea kuwa alikumbwa na ibilisi wa mapenzi, huku akiomba mahakama imwonee huruma kwa madai kwamba bado ni kijana na ana mke na watoto wanaomtegemea.

"Mheshimiwa Hakimu kwa vile mahakama imeshaniona nina hatia, naomba inionee huruma na sitarudia tena kosa la aina hii kwani ni ibilisi tu alinipitia," alijitetea.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John, alisimama na kuiomba mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia za aina hiyo, ikizingatiwa aliyemfanyia ukatili huo ni mtoto mdogo.

Pia John alidai kuwa unyama unaodaiwa kufanywa na mshtakiwa pamoja na ripoti na ushahidi uliotolewa na daktari, inaonyesha mtoto huyo alivyoumizwa na nguvu kubwa iliyotumiwa na mlalamikaji wakati wa utekelezaji wa tendo hilo.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Batraine kupitia vifungu 130 kifungu kidogo cha (1) kifungu (2) (a) pamoja na 131 kifungu kidogo cha (3) Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura 16 ya mwaka 2019, alisema amesikiliza maombi ya pande zote mbili na kueleza kutokana na sheria kumfunga mikono, anamhukumu mshtakiwa kifungo cha maisha jela. Licha ya kifungo hicho, mahakama iliamuru mshtakiwa kumlipa mlalamikaji fidia ya Sh. milioni tatu ili zimwezeshe kuendelea na matibabu kutokana na majeraha aliyoyapata sehemu za siri.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na mwanasheria John kuwa Agosti 24, mwaka huu, majira ya mchana, mshtakiwa akiwa anatambua kuwa kitendo anachokifanya ni kosa, alimbaka mtoto huyo kisha kumharibu sehemu za siri na kumsababishia maumivu makali.

Mwanasheria huyo alidai kwamba mshtakiwa alikamatwa na wananchi waliokuwa wakipita njia baada ya kusikia kelele za mtoto huyo na walipofuatilia, walimkuta (mshtakiwa) akijiandaa kuvaa nguo zake tayari kwa kukimbia baada ya kuona watu wakifuatilia kwenye eneo walilokuwapo na mlalamikaji.

## Asimulia alivyomwagiwa tindikali ugomvi wa mali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Mtaa wa Nyakato Kata ya Nyasubi, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Specioza Sylvester, amesimulia alivyomwagiwa tindikali akiwa jijini Mwanza baada ya kugombana na mumewe, Richard Majenga, alipotaka kugawana mali walizokuwa wakizimiliki.

Sylvester alitoa simulizi hiyo jana alipotembelewa na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, akimweleza alivyofanyiwa kitendo hicho na watu wasiojulikana na mume wake kuanza kuuza mali walizokuwa nazo zikiwamo nyumba, magari, viwanja na shule. Alisema alimwagiwa tindikali mwaka 2015 akiwa katika matembezi jijini Mwanza, alipokuwa amehamishia makazi yake baada ya kutengana na Majenga kutokana na mgogoro wa umiliki wa mali walizozitafuta walipokuwa wanaishi pamoja.

"Baada ya kupata madhara haya, familia yangu ilifanya uchunguzi na kubaini watu waliotekeleza tukio hilo walitumwa na mume wangu ili aniue na yeye amiliki mali tulizochuma pamoja. Nilipopona nilifuatilia suala hili kwenye vyombo vya sheria, lakini sikupata msaada," alisema.

Mwaka 2007, alisema walifunga ndoa na mwaka 2008 walijenga shule ya msingi (Jerusalemu) na nyumba mbili na mwaka 2013 iliibuka migogoro ndani ya ndoa na kuchukua hatua ya kuachana na mume wake kumuoa mwalimu wake aliyekuwa akifundisha katika shule hiyo na wanaishi pamoja mpaka sasa.

Kutokana na suala hilo, Waziri Nchemba ameiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kuchunguza upya shambulio la kumwagiwa tindikali kwa mwanamama huyo na kusitishwa kwa uuzwaji wa mali zinazomilikiwa baina yake na mumewe.

Dk. Nchemba alisema sheria na mahakama imechezewa vya kutosha, hivyo ni lazima hatua kali za kisheria zichukuliwe.

"Hakikisheni mnachunguza tukio hilo kwa kina na kunipatia taarifa na kuzuia uuzwaji wa magari unafanywa na Richard Majenga wakati bado kesi iliyofunguliwa dhidi yake ikiendelea kusikilizwa.

DERM GROUP

NOTICE OF HOLIDAY SEASON CLOSURE

Derm Group wishes to inform its esteemed clients and business partners that our offices (except for Derm Elevators Ltd) will be closed during the festive season with effect from **Friday 18th December 2020.**

Business will resume on **Monday 04th January 2021.**

Our operations in Bagamoyo, Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Mwanza, Tanga, and Zanzibar shall not be affected by this closure.

Any inconveniences caused is highly regretted.

We would like to thank all our clients and business partners in general for their continued patronage of our services throughout the year 2020.




DERM ELECTRICS (T) LTD — Electrical, HVAC, Security, ICT Contractors
SKYLINE PROPERTIES LTD
COAST CONCRETE POLES LTD
Derm Elevators
DTsmart

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ustawi jamii wabanwe ukaguzi wa 'Day Care'

**UWAPO** wa vituo vya malezi ya watoto (Day Care) umesaidia sana kuwapunguzia changamoto wazazi wengi ambao wamekuwa wakihangaikia malezi ya watoto wao wanapokuwa kazini na kwenye shughuli za biashara.

Wazazi wenye watoto wadogo hususan kinamama wamekuwa wakipata tabu kutokana na kutokuwa na uhakika kama watoto waliowaacha nyumbani wako salama ama wamepata huduma zinazotakiwa.

Wasiwasi huo hutokana na wasichana wasaidizi wa kazi wengi wao kutowajibika katika kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Kutokana na hali hiyo, kinamama huona ni muhimu kuwapeleka watoto kwenye vituo vya malezi, ambako kuna uhakika wa kupatiwa huduma bora na baada ya shughuli za kazi kuwakuta wakiwa salama. Mahitaji hayo ndiyo yaliyosababisha kasi ya kuanzishwa kwa vituo hivyo, kiasi kwamba vingine vinaanzishwa bila kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Yapo malalamiko kuwa kuna watu wamevianzisha katika mazingira hatarishi na yasiyo rasmi, huku mengine yakidaiwa kuwa vichochoroni, hivyo kwenda kinyume cha malengo ya kuanzishwa kwake.

Inawezekana wazazi wanasita kutoa taarifa za kulalamika pengine kutokana na vituo kutoza gharama ndogo. Hali hiyo inaonyesha kwamba baadhi ya mamlaka za serikali haziwajibiki, kutokana na kutochukua hatua.

Hata hivyo, tunaona kuwa hatua iliyochukuliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaweza kuweka sawa mambo, na kuvisanya vituo hivyo kuwa mahali salama kulelea watoto wetu.

Wizara hiyo imetoa siku 14 kwa wamiliki wa vituo hivyo, kurekebisha kasoro ili watoto hao walelewe katika mazingira sahihi na kwa kujibu wa sheria.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, alitoa agizo hilo jijini Arusha mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea baadhi ya vituo na kubaini kutozingatia masharti ya utoaji wa huduma kwa watoto kama ilivyoainishwa kwenye sheria na miongozo.

Alibaini kwenye kituo kimoja kuwa eneo lake halikidhi vigezo na mazingira ya kuwa kituo cha malezi ya watoto mchana, hivyo nawapa wamiliki wake wiki mbili warekebishe upungufu wote na mtafute eneo jingine.

Pia aliwaagiza maofisa ustawi kwenda kufanya ukaguzi baada ya siku 14, kama hawajakidhi serikali itakifunga, akisema huduma ya malezi kwa watoto inapaswa kuzingatia vigezo mbalimbali, ikiwamo vyumba vya madarasa, viwanja vya michezo na wahudumu wa kutosha na wenye sifa.

Alisema wizara imepanga kufanya operesheni maalum kwenye vituo hivyo nchi nzima, ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009.

Ushahidi wa ukiukwaji wa sheria unaofanywa vituo hivyo ulitolewa na baadhi ya wasimamizi wa vituo vilivyokaguliwa, kwamba vinaendeshwa kinyume cha utaratibu ikiwamo kutokuwa na usajili na mazingira yasiyofaa kwa malezi ya watoto.

Pamoja na Katibu Mkuu huyo kuwaagiza maofisa Ustawi wa Jamii kuvikagua vituo mara kwa mara ili kubaini kasoro na kuzitafutia ufumbuzi, bado tunasisitiza kuwa uwekwe utaratibu wa kuwabana maofisa hao kufanya ukaguzi huo.

Ikiwezekana kila baada ya miezi mitatu au sita, vinginevyo, wengi hawatafanya hivyo kutokana na utendaji wa kimazoea wa kukaa maofisini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vita ukatili jinsia, tunapaswa kuwa pamoja kusaka suluhu

Na Yasmine Protace

**NENO** ukatili limekuwa likitajwa karibu kila siku, kupitia vyombo mbalimbali vya habari na hata watu mbalimbali utasikia wanazungumza mtu kafanyiwa ukatili.

Ukatili upo na umekuwa ukifanywa na baadhi ya watu kwa kuwafanyisha watoto, wanawake na hata watu wa jinsia tofauti madhila tofauti.

Sababu za ukatili huo zimekuwa zikitajwa kwa namna tofauti kwamba upo ukatili wa kupigwa, wa kingono, maneno na hata kibiashara.

Ni baadhi ya mfano wa matukio ya ukatili. Muhimu ni jamii kuwa na nguvu ya pamoja ili kuutokomeza, katika nguvu ya pamoja kusaka mafanikio. Tunapozungumzia nguvu ya pamoja, tunamaanisha kuwa hata wanapofanyiwa matukio ya ukatili, wanapaswa watoe taarifa ili wahusika wachukuliwe hatua stahiki kisheria. Na wale wanapofanyiwa ukatili watoe taarifa, ni muhimu kutoa ushirikiano, hasa pale zinapofunguliwa ili mtuhumiwa akipatikana, hatua ichukuliwe.

Kama jamii ikisimama vizuri kusonga mbele, walalamikaji na mashahidi wakajitokeza mahakamani, ni hali itakayosaidia kuondokana na ukatili, kwa sababu kuna hatua ya kusonga mbele kufikia mafanikio ya ukomeshaji.

Katika kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia, serikali imeanzisha jumla ya kamati 16,313 ambazo zipo kila kona ya nchi, kwa ajili ya kupambana na matukio ya ukatili.

Dalius Demasi, Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, jijini Dar es Salaam. Demasi anasema, katika viwanja vya TGNP Mtandao, kwamba kuanzishwa kamati hizo kila kona ni mikakati ya kupambana na ukatili.

Anaongeza kuwa serikali imetekeleza mpango wa kupambana na ukatili ambao mpango huo upo katika ilani na serikali imefanya jitihada mbalimbali kuanzisha mafunzo ya kuwalinda wanawake na watoto dhidi ya matukio ya ukatili.

Ofisa huyo wa Ustawi wa Jamii, anaongeza kuwa katika kupambana na matukio ya ukatili madawati ya kusikiliza matukio hayo yameanzishwa Magereza, Polisi na vyuo vikuu, lengo ni kupata taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia na kuyashughulikia.

"Mbali na kuanzishwa kwa madawati magereza, polisi na vyuo, pia wameanzisha madawati katika baadhi ya shule, ili wanafunzi waweze kutoa taarifa pale wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia," anasema.

Anna Makinda, mgeni rasmi katika maadhimisho hayo ambayo asasi ya TGNP Mtandao hivi karibuni iliyaadhimisha katika mkzi yao, anasema katika kutokomeza ukatili unatakiwa kuwapo nguvu ya pamoja.

Mama huyo aliyewahi kuwa Spika wa Bunge nchini, anasema kila mmoja katika nafasi yake anatakiwa kupaza sauti, ili kuhakikisha ukatili huo unatokomea.

"Kila mmoja katika nafasi yake apaze sauti ya kuzungumzia ukatili wa kijinsia, kwani kutokomeza ukatili wa kijinsia ni kulinda haki za binadamu," anasema.

Anaeleza kuwa, Taifa lisilo na ukatili wa kijinsia ndilo lenye maendeleo na haki za binadamu ni lazima zizingatiwe, hivyo usalama wa wanawake na watoto ni muhimu sana katika kuwalinda dhidi ya ukatili.

Mama huyo anautafsiri ukatili wa kijinsia unaigharimu dunia, huku akitaja takwimu za kitaifa za mwaka 2015/2016, kwamba kuna asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 na 49, walishafanyiwa ukatili wa kipigo na ngono.

Anaitaja mikoa ya Kagera, Mwanza na Kigoma kuna matukio ya ukatili yanayoongezeka katika jamii na inatakiwa elimu muhimu kupunguza ongezeko la ukatili wa kijinsia.

Hadi sasa serikali imeshatekeleza mikakati ya kupambana na matukio ya ukatili, akirejea lengo la mwaka 2022 linanuia kufika mbali kupunguza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto na Makinda anaongeza kuwa, ni hali inayokwaza uchumi nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Liliani Liundi, anasema kuwa Kampeni ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia ya Siku 16 Kitaifa, anatoa mfano wa kwingineko kwamba kuna historia wanawake watatu kutoka visiwa vya Dominika, waliuawa baada ya kupinga ukatili kwa jinsia yao.

Anasema mwaka 1999 duniani ilipitishwa rasmi Siku ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia, katika kupambana na matukio ya ukatili duniani na jamii inatakiwa kuwa mstari wa mbele kupinga.

"Wanapofanyiwa ukatili wengi wao, hawazifikii ndoto zao ambazo walikuwa wamejipanga hapo baadaye walitaka wawe kina nani," anasema.

HABARI KITAIFA

# Mwambe, bosi Standard Chartered wamlilia Patel

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe anatoa salamu za pole kwa familia, ndugu jamaa na marafiki kutokana na kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa Motisun Group, Subhash Patel, huku akisema taifa limempoteza mwana- viwanda na mzalendo wa kweli.

Katika taarifa ya wizara iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, Mwambe alisema Patel alitoa mchango mkubwa katika kufikia malengo ya nchi ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mwambe, kupitia taarifa hiyo, alisema mfanyabiashara huyo alijikita katika sekta mbalimbali za viwanda akiwa na lengo la kuhakikisha bidhaa muhimu zinapatikana nchini bila kuagiza kutoka nchi za nje. Viwanda vyake vingi vinazalisha bidhaa za ujenzi kama vile nondo, mabati, rangi, mabomba, matangi na vinywaji.

Mbali na viwanda, Patel alijihusisha pia katika huduma za ukarimu kwa kujenga na kuendesha hoteli na nyumba za kupangisha pamoja na kupanua wigo wa biashara kwa kuanzisha na kuendesha viwanda katika nchi za jirani kama vile Msumbiji, Uganda na Zambia.

Kwa Tanzania, alianzisha na kusimamia uendeshaji wa viwanda MMI Steel (vya nondo na mabati), MM Industries cha mabomba na matangi ya kiboko, Kiboko Paints, Sayona Drinks cha Dar es Salaam, PNP Industries cha vyuma na mabati, Kiboko Pre-Coated Sheets (mabati ya rangi), kiwanda cha matunda cha Sayona Fruits - Mboga Chalinze na Sayona Drinks - Mwanza. Viwanda vilivyojengwa nje ni vye MMI Steel Uganda, Msumbiji na Zambia.

Mbali na viwanda hivyo, taarifa hiyo ilisema mwanaviwanda huyo nguli alikuwa katika mchakato wa kuanzisha miradi ya kuchimba Makaa ya Mawe Katewaka - Ludewa kupitia Kampuni ya Maganga Matitu Resource Development Limited, kiwanda cha saruji Mamba, Bagamoyo na kiwanda cha Soyona - Mbeya.

Katika huduma za ukarimu, Patel alianzisha na kuendesha hoteli za Whites Sands, Sea Cleaf na Sea Cleaf Apartment zilizopo Dar es Salaam na Sea Cleaf Zanzibar pamoja na mgawaha wa Best Bite, Namanga, Dar es Salaam.

"Subhash Patel alikuwa mfano wa kuigwa kwa wengi wetu hasa katika ujenzi wa uchumi unaoongozwa na viwanda. Amekuwa mstari wa mbele kutoa ushauri kwa wana viwanda wenzake kwenye vikao vyetu vya wadau wa viwanda," ilisema taarifa hiyo.

**BOSI STANDARD**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, amemwelezea marehemu Subhash Patel, kwamba alikuwa mtu aliyekuwa na mchango mkubwa kwenye maendeleo ya taifa.

Amesema Patel enzi za uhai wake aliwahamasisha vijana, viongozi na jamii kwa ujumla katika masuala ya maendeleo.

Vilevile, amesema Patel kwamba alikuwa nguzo muhimu kwa sekta binafsi, kimaendeleo na kuisaidia kupiga hatua kwa zaidi ya miongo kadhaa.

Rughani ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wakurugenzi wa kampuni nchini (CEO Roundtable), alimwelezea Patel kuwa alikuwa mfanyabiashara mkubwa nchini.

# BAWACHA yawajia juu kina Mdee

**Na Maulid Mmbaga**

BARAZA la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), limewajia juu Halima Mdee na wenzake 18 waliofukuzwa, kwa madai ya kutumia nyaraka, nembo na bendera za chama kujisafisha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA Zanzibar, Sharifa Suleiman, wamebaini kuwa wabunge hao wanashirikiana na mamlaka za waliodai ni watesi wao kwa kuandaa kongamano la wanawake.

Alisema wabunge hao si viongozi wala wanachama wa CHADEMA tangu Novemba 27, mwaka huu, walipovuliwa nafasi zao na kufukuzwa uanachama kwa kushiriki mambo aliyodai haramu.

Sharifa alisema wabunge hao wanatumia nembo na jina la CHADEMA kuwahadaa na kughiribu baadhi ya viongozi na kinamama wa BAWACHA kwa fedha, ili wafike Dar es Salaam kwenye mkusanyiko wanaouandaa kwa jina la wanawake wa CHADEMA.

"Katika hatua hii ya awali, tunawapongeza kinamama na viongozi wa BAWACHA waliokataa hadaa na hongo walizopewa au kuahidiwa. Tunatambua wako wanawake ambao wamewajibu pasipo shaka na kuwaambia kuwa hawana tena mamlaka ya kuwaita kwa jambo lolote linalohusu CHADEMA na hawana hadhi ya kushirikiana na wanachama katika masuala yanayohusu CHADEMA kwa sababu si wanachama wa chama hiki tena wala baraza letu," alisema.

Pia alisema wanaendelea kufuatilia nyendo za wabunge hao, ikiwamo kuchukua hatua za haraka kwa kuzuia matumizi mabaya ya nembo za BAWACHA na CHADEMA ikiwa mwendelezo wa alichodai ni uhalifu dhidi ya taratibu za kisheria zinazohusu chama.

Alisisitiza kuwa viongozi wa baraza katika ngazi ya mkoa, wilaya, majimbo na kata kwamba BAWACHA na CHADEMA hawajaandaa kongamano lolote la wanawake.

Sharifa aliwataka wanawake wa BAWACHA na CHADEMA kwa ujumla kuwa imara wakati wakiendelea kujipanga kwa ajili ya kutekeleza maazimio ya kamati kuu, ikiwa ni pamoja na kuziba nafasi za waliofukuzwa.

"Tuzidi kuwa imara kama jadi yetu kwa kusimama na chama chetu pia kufahamishana kuwa uamuzi wa kuwafukuza uanachama Halima Mdee na wenzake 18 unaendelea kutamalaki, kutekelezwa na haujabadilika.

"Mwanachama au kiongozi yeyote atakayeshirikiana na watu hao katika mienendo yao, atambue atakuwa anakiuka taratibu na maamuzi ya chama na atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa katiba ya chama na mwongozo wa BAWACHA," alisema.




# CRDB yamwaga zawadi ya funga mwaka

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetoa zawadi kwa wanafunzi wa vyuo mbalimbali nchini ikiwa ni sehemu ya kampeni ya JIPE 5 ambayo ilizinduliwa Oktoba, mwaka huu, ili kuhamasisha Watanzania kujiwekea akiba kuelekea mwisho wa mwaka.

Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi wa CRDB, Abel Lasway, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa hadi jana, benki tayari imeshatoa zawadi zinazofikia Sh. milioni 20. Zawadi hizo zimetolewa kwa zaidi ya wateja 4,000 huku zaidi ya akaunti 74,000 zikiwa zimekwisha funguliwa.

“Tunawashukuru sana Watanzania kwa kuipokea vyema kampeni ya Jipe Tano. Mafanikio yaliyopatikana si tu ni kwa faida ya CRDB bali yanaonyesha ni kwa jinsi gani benki imeweza kuwajumuisha Watanzania wengi katika mfumo rasmi wa huduma za fedha,” alisema Lasway.

Meneja huyo alisema katika kampeni hiyo ya Jipe Tano, makundi mbalimbali ya wateja yamezawadiwa na kwa mwezi huu, Benki inawazawadia ada za shule wazazi wanaofungua akaunti ya watoto za Junior Jumbo. Alisema jumla ya Sh. milioni 30 zimeandaliwa kwa ajili ya kutolewa kama zawadi ya ada kwa akaunti za watoto za Junior Jumbo zitakazofunguliwa mwezi Desemba.

“Benki ya CRDB tunajinasibu kwa kaulimbiu yetu ya “Ulipo Tupo” ambayo haiishii tu kufikisha huduma mahali ambapo wateja wetu wapo bali inalenga kuhakikisha benki inakua pamoja na mteja katika hatua zote za maisha yake,” aliongezea Lasway.

Sambamba na zawadi hizo kwa akaunti za akiba na watoto, alisema CRDB pia ililenga kundi la wanafunzi wa vyuo ambavyo vimefunguliwa hivi karibuni. Timu ya mauzo ya benki iliweka kambi katika vyuo mbalimbali, ili kutoa elimu ya masuala ya fedha na kutoa huduma za kufungua akaunti kwa wanafunzi.

Akizungumza baada ya kutangazwa kuwa mshindi wa ‘laptop’ (kompyuta mpakato), Jackline Masayanyika, mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, jijini Mwanza, alisema kuwa zawadi hiyo itakuwa msaada mkubwa katika masomo yake ikizingatiwa uwapo wa fursa nyingi za masomo zinazopatikana mtandaoni.

# Hukumu kesi ya mauaji ya Mawazo wiki ijayo

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita inatarajia kutoa hukumu ya kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Geita na mgombea ubunge Jimbo la Busega, Alphonce Mawazo (pichani) Desemba 24, mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Msajiri Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza ambaye ni Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya Ziada (Extended Jurisdiction), Frank Mahimbali.

Hakimu Mahimbali alisema hayo baada ya upande wa Jamhuri na wa utetezi kumaliza kutoa ushahidi wao.

Upande wa Jamhuri ulipeleka mashahidi 13 na vielelezo nane, huku upande wa utetezi ukipeleka mashahidi watatu na vielelezo vitatu.

Hakimu Mahimbali alisema jana kuwa kabla ya kutoa uamuzi huo, Desemba 23 wazee washauri watatoa maoni yao.

Awali, mshtakiwa wa tano katika kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Gerita na mgombea ubunge Jimbo la Busanda mwaka 2015, Alphonce Mawazo, Kululinda Bwire (38) mkazi wa Katoro, amekana kuhusika.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Paul John, mshtakiwa alidai Novemba 14, mwaka 2015 niliondoka majira ya saa 2 asubuhi kuelekea ofisi ya mtendaji wa kata ya Katoro kwa ajili ya kuhudhuria semina ya mawakala kwa ajili ya kusimamia uchaguzi mdogo wa udiwani wa Kata ya Rudete.

Bwire alidai mahakamani juzi jioni kuwa wakiwa ofisi ya mtendaji huyo, ilionekana eneo hilo ni dogo na halitoshi kufanyia semina wakaambiwa waende katika shule ya sekondari.

Aidha alisema, walipewa viapo vya kutunza siri pamoja na fomu namba 6, ambayo aliomba mahakama iipokee kama kielelezo.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Mwenye Mamlaka ya Ziada, Mahimbali alipokea fomu hiyo kama kielelezo na kuipa alama ya namba 3.

Mshtakiwa alidai baada ya kumalizika semina alirudi nyumbani na ilipofika majira ya saa 12:30, alielekea kijiweni kunywa kahawa, lakini akiwa hapo alikisia taarifa za kifo cha Mawazo, na kwamba baada ya kusikia hivyo alirudi nyumbani kwake eneo la Katoro.

Alidai Novemba 15, 2015 aliamka asubuhi majira ya saa 2 na kwenda kusimamia uchaguzi hadi saa mbili usiku na walirudisha maboksi kwenye ofisi ya mtendaji kisha kurudi nyumbani kwake.

Aliendelea kuieleza mahakama kuwa Novemba 16, 2015 akiwa kwenye shughuli zake, aliwaona watu wawili ambapo mmoja alikuwa na bunduki wamevaa kiraia na kumwambia anahitajika Kituo cha Polisi Buselesele, na kuondoka na gari hadi kituoni kisha walimweka mahabusu hadi majira ya saa tatu usiku walimtoa na kuanza kumhoji, na kuandika maelezo yake.

Aidha, Bwire alidai Novemba 17, 2015 askari polisi walimwambia anatakiwa akawapeleke nyumbani kwake, na walipofika walimwambia awaonyeshe nguo alizokuwa amezivaa Novemba 14, 2015.

“Niliwapatia tisheti moja, suruali moja aina ya kaki na viatu pea moja vyenye rangi mchanganyika, na baada ya kuwapatia vitu hivyo tulirudi Kituo cha Polisi Buselesele, na ilipofika majira ya saa 10 jioni walinipeleka kituo cha polisi Geita,” aliiambia mahakama.

Aliongeza kuwa Novemba 18, 2015 alitolewa mahabusu na kupelekwa kwenye gwaride la utambulisho majira ya saa 2 asubuhi, ambapo shahidi wa Jamhuri, Saidi Omary, alimtambua kwa kumshika bega mbele na nyuma.

Baada ya utetezi kumaliza kumwongoza mteja wake, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Mkuu Javelin Rugaihuruza, ulimhoji mshtakiwa kama ifuatavyo:

**Wakili:** Ebu tueleze chakula cha mchana ulikula nyumbani kwako?

**Shahidi:** Sikula cha mchana nyumbani.

**Wakili:** Kilichoanza ni kiapo au semina?

**Shahidi:** Ni semina.

**Wakili:** Wewe ulikuwa wakala wa chama gani?

**Shahidi:** Wa Chama Cha Mapinduzi.

**Wakili:** Kwenye semina ulikuwa na nani?

**Shahidi:** Sikumbuki.

**Wakili:** Mke wako anaitwa nani?

**Shahidi:** Anaitwa Magdalena Mgemo.

**Wakili:** Ni kweli uliwapatia polisi nguo na viatu?

**Shahidi:** Ndiyo niliwapa.

**Wakili:** Wewe ni mwanachama wa CCM?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Umeleta picha za pasipoti ulizojaza kwenye usimamizi hapa mahakamani?

**Shahidi:** Sijaleta.

**Wakili:** Mhuri uliyozajazwa kwenye hati ya usimamizi umeandikwaje?

**Shahidi:** Tume ya uchaguzi.

**Wakili:** Wewe gerezani una cheo gani?

**Shahidi:** Cha katekista.

**Wakili:** Ulipokamatwa ulipelekwa wapi?

**Shahidi:** Kituo cha Polisi Buselesele.

**Wakili:** Nguo ulizowapa polisi ulikuwa umeziweka wapi?

**Shahidi:** Zilikuwa chini ya cherehani.

**Wakili:** Wakati unaandika maelezo yako polisi ulisainishwa?

**Shahidi:** Ndiyo nilisaini.

**Wakili:** Wakati wewe mnafikishwa mahakama ya wilaya uliposomewa shtaka lako la mauaji ulikana?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Wakati unachukuliwa maelezo polisi ulipigwa?

**Shahidi:** Sikupigwa.

**Wakili:** Semina hiyo iliisha saa ngapi?

**Shahidi:** Iliisha saa 6 mchana.

**Wakili:** Je, umeonyesha kitabu cha mahudhurio hapa mahakamani?

**Shahidi:** Sikuleta.

**Wakili:** Ulipewa posho kiasi gani?

**Shahidi:** Nilipewa Sh. 24,000.

**Wakili:** Muhtasari wa kikao unao hapa mahakamani?

**Shahidi:** Sikuleta, sina.

**Wakili:** Kwenye semina mlikuwa watu wangapi?

**Shahidi:** Tulikuwa wengi.

**Wakili:** Ulimfahamu lini mshtakiwa Epafula Zacharia?

**Shahidi:** Kwenye semina ya uwakala na usimamizi wa uchaguzi mdogo wa udiwani Kata ya Rudete.

**Wakili:** Ulipokamatwa uliweka wapi fomu ya usimamizi?

**Shahidi:** Mfukoni nikaingia nayo mahabusu.

**Wakili:** Ulikabidhi hati ya usimamizi ya uwakala Magereza?

**Shahidi:** Hapana.

**Wakili:** Fomu ya uwakala na fomu ya kiapo ni sawa?

**Shahidi:** Mimi sijui.

**Wakili:** Wewe uliteuliwa na chama au mgombea?

**Shahidi:** Niliteuliwa na CCM.

**Wakili:** Barua ya kuteuliwa iko wapi?

**Shahidi:** Sina.

Baada ya upande wa Jamhuri kumaliza kumhoji, upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Paul John, ulimhoji mshtakiwa Bwire kama ifuatavyo:

**Wakili:** Utofauti wa mihuri unasemaje?

**Shahidi:** Mimi sijui suala hilo.

Wakili: Gwaride la utambuzi uliridhika?

**Shahidi:** Sikuridhika.

Baada ya mshtakiwa huyo kumaliza kutoa utetezi wake, Wakili John alidai ana shahidi mmoja wa mshtakiwa na yuko tayari kutoa ushahidi wake.



Hakimu Mahimbali alikubaliana na ombi hilo na kuanza kusikilizwa. Shahidi wa mshtakiwa huyo, Modesta Magesa (43), Mwalimu wa Shule ya Msingi Mkapa na mkazi wa Katoro, akiongozwa na Wakili John, alidai Novemba 14, 2015 majira ya asubuhi alienda kwa mtendaji wa Kata ya Katoro na kulikuwa na watu wengi.

Kwamba baada ya kufika ilionekana kuwa eneo la kuwapisha mawakala ni dogo, hivyo mtendaji aliamua kwenye Shule ya Sekondari Katoro.

Alidai zoezi hilo lilimalizika majira ya saa 9 jioni wakatawanyika na kurudi majumbani mwao.

Baadaye upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Rugaihuruza, ulimhoji shahidi Magesa kama ifuatavyo:

**Wakili:** Wewe ulikuwa na wadhifa gani?

**Shahidi:** Msimamizi.

**Wakili:** Hiyo barua ya kuteuliwa kuwa msimamizi ulileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Hapana.

**Wakili:** Ili wakala aweze kuja kwenye uchaguzi anatakiwa awe na nini?

**Shahidi:** Barua kutoka kwenye chama cha siasa.

**Wakili:** Siku ya kuapishwa ulikuwa chumba kimoja na mawakala?

**Shahidi:** Hapana tulikuwa na chumba chetu, na mawakala chumba chao.

**Wakili:** Tukio la kuuawa Alphonce Mawazo ulilisikia lini?

**Shahidi:** Novemba 14, 2015 majira ya jioni.

**Wakili:** Wewe unafahamu mshtakiwa wa tano Kululinda Bwire ni mwanachama wa chama gani?

**Shahidi:** Wa CCM.

**Wakili:** Wewe ni mwalimu wa taaluma?

**Shahidi:** Hapana.

Washtakiwa hao ni Alfan Apolinari (41), Epafula Zacharia (39), Hashimu Sharifu (45) na Kululinda Bwire (31) wote kwa pamoja ni wakazi wa Katoro mkoani Geita.



Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba (kulia), akikagua mashamba ya wakulima wa zao la kahawa katika Kata ya Upolo, Tarafa ya Mpepo, wilayani humo, huku akiwataka wakulima kuongeza uzalishaji wa zao hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mufti afichua siri ya maelewano Zanzibar

**Na Suleiman Omar**, PEMBA

MUFTI wa Zanzibar, Sheikh Swalehe Omar Qaabi, amesema subira, imani na kushiba kwao dini kwa watu wa Zanzibar, ndiko kunakosababisha kuwapo kwa imani inayojenga maelewano hata pale wanapohitilafiana katika mambo ya kidunia.

Mufti Qaabi aliyasema hayo jana, Wesha, nje kidogo ya mji wa Chake Chake alipokuwa akilifungua kongamano la siku moja lililowashirikisha masheikh na viongozi wa vijana wa kiislamu kisiwani Pemba.

Alisema kutokana na makubaliano ya kumaliza tofauti baina ya Wazanzibar kumewapa nafasi mataifa mbalimbali barani Afrika kufika Zanzibar kuona na kujifunza wanavyoweza kumaliza matatizo yao pasi kuingiliwa na mataifa ya nje.

Aliwasihi viongozi wa dini kuendelea kuzitawala nyoyo za wafuasi wao kuziweka katika hali ya kujenga imani zao kumwogopa Mwenyezi Mungu, ili kujiepusha na matendo ambayo yanaweza kuwaingiza katika maangamizi.

Akizungumza na viongozi hao, Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Issa Juma Ali, aliwataka kukaa pamoja na jamii zao kuwahimiza kuitunza amani iliyopo na kuwataka watu waishi kwa kuelewana ili amani iendelee kudumu. Issa aliwataka kudumisha utamaduni, mila na silka zilizopo na kuacha kufuata mila na utamaduni wa mataifa mengine ambayo yanaweza kuharibu mustakbali mzima na kusababisha matatizo ambayo yanaweza kuibua machafuko.

Awali, Katibu wa Jumuiya ya Marafiki wa Kweli wa Zanzibar, Abubakar Kabwogi, aliwapongeza Wazanzibari kwa kuonyesha ukamavu ndani ya Afrika na duniani kote kwa kumaliza tafauti zao.

Kabwogi alisema jambo hilo litayafanya mataifa mengi kufika Zanzibar na kujifunza namna tofauti zinavyotatuliwa bila kusababisha maafa. Alisema kinachotokea Zanzibar nafasi yake katika kujenga amani Afrika Mashariki.

Alisema kunakuwa na migogoro mingi na kwa muda mrefu kwa baadhi ya nchi kama vile Msumbiji kati ya chama tawala na RENAMO na wahusika kushindwa kutatua badala yake kutatuliwa Roma.

Pia alisema Malawi pamoja na udogo wake, mgogoro wake ulitikisa mpaka wakaenda Afrika Kusini wakasuluhishwa. Burundi nayo alisema ilihangaika mpaka mgogoro wake ukasuluhishwa Arusha. "Nakwambieni jamani mfano huu uliofanywa na watu wa Zanzibar, kuna watu hawalipendi hili," alisema.

Aliwasihi wa Zanzibar wahimizane kutunza amani iliyopo isichezewe na isiwe mradi bali ifanywe kuwa mila, silka na utamaduni wa kila Mzanzibari na kuwafanya watu kuja kungalia.

Kongamano hilo lilihudhuriwa pia na Naibu Mufti wa Zanzibar, Mahmoud Mussa Wadi na viongozi wengine wa dini na serikali.

# Ahueni huduma tiba ya saratani KCMC

**Na Mwandishi Wetu**, MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya KCMC, imewapunguzia mzigo wagonjwa wa saratani wanaotokea mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Kati na nchi jirani, kusafiri umbali mrefu kufuata tiba hiyo jijini Dar es Salaam.

Hatua hiyo inatokana na hospitali kuzindua wodi ya saratani yenye uwezo wa kuchukua wagonjwa 47 kwa wakati mmoja.

Ujenzi wa wodi hiyo umetumia Sh. bil. 1.8 hadi kukamilika kwake. Kiasi kikubwa cha fedha hizo kimetolewa na wafadhili kutoka Foundation For Cancer Care in Tanzania (FCCT), ikishirikiana na Shirika la Msamaria Mwema (GSF).

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Prof. Gileard Masenga, jana alimweleza Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fedrick Shoo, wakati wa hafla ya uzinduzi wa wodi hiyo yenye vyumba 10 kwamba hata watumishi wa hospitali hiyo wamechangia ujenzi kwa kukatwa asilimia mbili katika mishahara yao.

"Tunamshukuru Mungu kwa jengo hili na vifaa tulivyokuwa navyo, ila tatizo kubwa ni wataalamu wa kuwahudumia wagonjwa watakaokuwa wamelazwa katika wodi hii. Kwa sasa tumeomba serikali kutupatia wafanyakazi hao," alisema.

Aidha, alisema tatizo lingine linaloikabili kwa sasa ni kutokuwapo kwa huduma ya kutibu saratani kwa njia ya mionzi. Ujenzi wa jengo la mionzi yaani 'bunker for radiotherapy' pamoja na mashine inagharimu Sh. bilioni saba.

Katika hotuba yake, Prof. Masenga alisema wanaishukuru serikali kwa kuahidi kusaidia sehemu ya ujenzi wa jengo hilo la mionzi kwa kuchangia Sh. bilioni mbili. Kwa mujibu wa Prof. Masenga, tangu kuanzishwa kwa huduma ya saratani hospitalini hapo mwaka 2016, wagonjwa 24,823 wamepatiwa huduma na kati yao wagonjwa 2,945 ni wapya.

Askofu Dk. Shoo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Shirika la Msamaria Mwema linalomiliki KCMC, aliishukuru serikali kwa kulisaidia kanisa kwa sehemu kubwa watumishi wa hospitali hiyo, lakini kuahidi kuwawezesha fedha za kujenga jengo la tiba ya mionzi.

"Serikali yetu imeonyesha nia nzuri katika kuunga mkono jitihada za kanisa, kwa mchango wake wa huduma za afya hapa nchini, ni imani yangu kwamba serikali yetu sikivu itapokea ombi hili na kutuwezesha kufikia ndoto yetu ya kujenga jengo la mionzi.

Lakini nawashukuru sana marafiki zetu wa kule Marekani (Foundation For Cancer Care), Mission One World lakini vile vile ndugu zetu wa Kanisa la Bavaria kutoka nchini Ujerumani, kwa msaada mkubwa ambao wametupa wa vitanda na magodoro ya wodi nzima," alisema Dk. Shoo.

# Neema yanukia wakulima mkonge

**Na Mwandishi Wetu**

NEEMA inanukia kwa wakulima wa mkonge nchini baada ya Kampuni ya Mkonge ya Grosso kuweka wazi kuwa inatarajia kuwekeza Dola milioni 5.7 (Sh. bilioni 132.8) kwa ajili ya kilimo na viwanda vya zao hilo.

Kampuni hiyo yenye maskani yake Uholanzi, imeingia nchini kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya kilimo hususan zao hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Nuradin Osman, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, kuwa amebaini uzalishaji wa mkonge nchini hauna ufanisi kama inavyotakiwa kulinganisha na hali ilivyo duniani.

"Bado kuna pengo kubwa la uzalishaji, teknolojia hafifu na faida ndogo kwa wakulima, wawekezaji na wadau wengine katika sekta hiyo.

"Kutokana na hali hiyo, sekta haiwezi kuvutia soko la kimataifa, jambo ambalo linaathiri uchumi wa nchi.

"Mnyonyoro wa thamani wa zao hilo hautumiki ipasavyo kwani asilimia mbili ya nyuzi zinazopatikana na mazao mengine yote yanaachwa. Hali hii inapoteza faida ya zao hilo katika mnyororo wa thamani," alisema.

Osman alisema uwekezaji wao unakusudiwa kuwa katika vipindi viwili vikiwa na lengo la kufufua zao hilo lililokuwa miongoni mwa mazao makubwa ya kibiashara nchini.

"Kiasi cha Dola milioni 5.7 kitaingizwa kwenye ukuzaji wa zao la mkonge kwa kuanzisha viwanda vya kuchakata mkonge vitakavyoongeza thamani. Lengo letu ni kukuza thamani ya mkonge nchini," alisema.

Alisema awamu ya kwanza itajikita katika kuimarisha mfumo wa huduma kwa wateja.

Alisema kampuni itaanzisha mikakati ya kuunganisha wazalishaji ambao ni wakulima na wateja duniani kote.

"Kampuni itatoa Dola 700,000 katika awamu ya kwanza. Taarifa za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) zinaonyesha uzalishaji hautoshi na hivyo kuna haja ya kuwa na uzalishaji zaidi," alisema.

"Utekelezaji katika awamu ya pili utakuwa pamoja na kuanzisha mfumo wa kuongeza thamani katika sekta. Grosso Sisal inalenga kuongeza thamani ya zao la mkonge kwa kuzalisha vileo, vyakula vya wanyama na sukari itokanayo na mkonge na kemikali inayozalisha nishati," alisema.

## Chalamila asimamia ubomoaji nyumba ya aliyegoma

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesimamia zoezi la kubomoa nyumba ya Atony Lyuba, mkazi wa Kata ya Inyala, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, baada ya kukaidi agizo la kubomoa kwa hiari nyumba yake.

Uamuzi wa Mkuu wa Mkoa, ulitokana na Lyuba kukaidi agizo la kupisha mradi wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 16.7 ambao unajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Inyala hadi eneo la Simambwe, baada ya viongozi mbalimbali wa serikali kumtaka avunje nyumba yake kwa hiari na kugoma.

"Nimeamua nije mwenyewe kubomoa nyumba yako, maana kila wakati tulikuomba kwa hiari yako, lakini uligoma, haiwezakani wenzako wote wakubali kubomoa halafu wewe peke yao ugome kama ni imani za kishirikina basi tutaziona," alisema Chalamila.

Mkandarasi wa mradi huo, Imelda Ngailo, alisema hatua ya Lyuba kugoma kubomoa nyumba, kumecheleweshwa ya shughuli ujenzi kwa kuwa nyumba yake kuwa katikati ya hifadhi ya barabara.

Alisema mradi huo ulianza mwezi Aprili, mwaka huu na ulitakiwa kukamilisha Desemba, lakini kutokana na kikwazo hicho utachelewa kukamilika kwa mujibu wa mkataba.

Baadhi ya wananchi walipisha mradi huo walipongeza hatua ya serikali kubomoa nyumba hiyo na sasa ujenzi utaendelea kama kawaida.

Miongoni mwa wakazi hao, John Moses, alisema walishangazwa na kitendo cha Lyuba kugoma kubomoa nyumba yake ambayo ilikuwa katika hifadhi ya barabara ilhali wao walikwishachukua uamuzi.

Kwa upande wake, Lyuba alikanusha madai ya yeye kugoma kubomoa nyumba na kuwa hakuna kiongozi yeyote aliyemfuata kumpa maelekezo.

"Hakuna mwenyekiti wa kijiji wala kata aliyekuja kwangu kuniambia nibomoe nyumba zaidi nikifika ofisini kwako mkuu wa mkoa na nikaamuriwa kuwa niko chini ya ulinzi kwa kukaidi agizo la kubomoa kwa hiari nyumba yangu," alisema Lyuba.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (kushoto), akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi (DED), Justice Kijazi (kulia), ilani ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2020-2025, kwa ajili ya utekelezaji, wapili kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ally Mwanga na Makamu Mwenyekiti, Jumanne Iddi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SGA yashinda tuzo ya ulinzi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya SGA Security imeibuka mshindi wa jumla kama kampuni yenye rasilimali za kutosha na ya kuaminika (Most Equipped and Reliable Security Company of the Year, 2020) katika tuzo za chaguo la wateja zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

SGA Security ilikuwa inachuana na kampuni nyingine saba za ulinzi ambapo wateja walitakiwa kupiga kura kwa njia ya mtandao kwa muda wa mwezi mmoja kuanzia Novemba 5, mwaka huu.

Baada ya kutangazwa washindi, baadhi ya walinzi wa SGA Security waliibuka kwa furaha, huku wakimsindikiza Mkurugenzi wao, Eric Sambu katika jukwaa kuu kupokea tuzo hiyo.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Sambu alisema imekuja wakati mwafaka ambao SGA inaadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwake, ikiwa ni kampuni ya kwanza ya ulinzi kusajiliwa nchini kiitwa Group 4 Security (T) ikiajiri zaidi ya wafanyakazi 6,000 kwa sasa.

"Tuzo hii tunawatunuku wateja wetu kwa kuwa na imani kwetu kwa huduma tunazotoa. Hii inatupa motisha kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kuhakikisha wanaona thamani ya fedha wanazolipa," alisema Sambu.

Aliwapongeza wafanyakazi wa SGA kwa kuifanya kampuni iwe bora zaidi kutokana na utendaji wao uliotukuka. "Kuna kampuni zaidi ya 2,000 za ulinzi nchini, lakini kinachotutofautisha nao ni jinsi tunavyotoa huduma kwa wateja. Tuzo hii inadhihirisha kuwa tunaelewa wanachohitaji wateja na tunaelewa namna ya kuwapa huduma hizi. Tunatoa kipaumbele kwa wafanyakazi, ili waendelee kutoa huduma bora na kukidhi matarajio ya wateja," alisema.

Meneja Masoko wa SGA, Faustina Shoo, alisema kwao ni furaha kupokea tuzo hiyo hasa katika mwaka uliokuwa na matatizo mengi likiwamo janga la Covid-19.

"Sisi SGA tuliweka umuhimu wote kwa mteja na tuliwapa kipaumbele na kwa pamoja tuliweza kulishinda janga hili tunawashukuru kwa kweli," alisema.

SGA Security inatoa huduma mbalimbali ikiwamo za ulinzi, tahadhari (alarm), huduma za fedha, ulinzi wa kielektroniki na kusafirisha mizigo. Sambu alisema kampuni hiyo pia inajivunia ushirikiano na Jeshi la Polisi hasa katika masuala ya mafunzo, udahili na pia katika operesheni za pamoja.

Alisema wamepania kushinda tuzo hiyo tena mwakani, huku akiwashukuru waandaaji kwa namna walivyoendesha zoezi hilo la kuwapata washindi kwa kutoa fursa kwa wateja kuchagua hivi kufanya tuzo hizi kuwa bora zaidi na za kuaminika katika ukanda huo kwa kuwa itakuwa chachu kubwa ya utoaji wa huduma zenye ubora wa juu.

# HakiElimu yataka wanafunzi kugundua vipaji, kuvitumia

**Na Gwamaka Alipipi**

WANAFUNZI wa kidato cha tano na sita wametakiwa kugundua vipaji vyao na kuvitumia katika kutatua kero zilizopo katika jamii, kwamba kupitia vipaji walivyonavyo wana uwezo wa kuleta mabadiliko na maendeleo nchini.

Rai hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya HakiElimu, John Kalaghe, wakati wa ugawaji tuzo ziitwazo Uwezo, zilizoandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Great Hope Foundation, kusema kuwa vijana wananguvu ya kuleta mabadiliko katika jamii kupitia uvumbuzi.

"Wanafunzi wa sekondari wananafasi kubwa ya kuleta mabadiliko katika jamii na nchi kwa ujumla, lakini kwanza wanatakiwa kuanza kugundua vipaji walivyonavyo na kuvitumia," alisema Kalaghe. Kalaghe alieleza kuwa wanafunzi wa sekondari hususani wa kidato cha tano na sita ndiyo wanaopaswa kuleta mabadiliko ya namna jamii inavyopaswa kuishi kupitia vipaji vyao halisi.

Tuzo za Uwezo zimebuniwa na Shirika lisilo la kiserikali la Great Hope Foundation (GHF), zikiwa na lengo la kubaini vipaji vya wanafunzi wa sekondari, namna ya kuviendeleza kupitia mashindano ya ubunifu kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Kwa mwaka huu, washindi wa tuzo hizo ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Wanaume Kibaha, Shule ya Sekondari ya Benjamin William Mkapa, pamoja na Shule ya Sekondari ya Hananasif. Kalaghe alisema wanafunzi wa sekondari wanapaswa kutosubiri hadi uzee wao ndipo waanze kujihusisha na masuala ya kijamii, bali wanapaswa kuanza sasa, ili kuikomboa jamii.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Great Hope Foundation (GHP) nchini, Noelle Mahuvi, alisema kwa mwaka huu shule zilizoshiriki kwenye shidano hilo zilikuwa 140 kutoka Dar es Salaam na Pwani.

Alisema kati ya idadi hiyo ni shule 35 ambazo zilipewa tuzo mbalimbali ikiwamo tuzo ya dhahabu, fedha, shaba, kwamba tangu mwaka 2016 wanafunzi kutoka shule mbalimbali wamekuwa wakipata tuzo. Alisema: "Mafanikio makubwa katika kuendesha tuzo za Uwezo ambayo tumeyashuhudia ni kuona wanafunzi wanajengewa ujuzi na ujasiri wa kufanya ujasiriamali. Tumeshuhudia watoto ambao walikuwa washiriki miradi mbalimbali ya tuzo hizi hasa wale waliokuwa viongozi wakijiingiza katika ujasiriamali."

Aliongeza: "Na kwa kuliona hili, Taasisi ya Great Hope Foundation, mwakani imekusudia kuanzisha tuzo nyingine zitakazoenda kwa jina la Uwezo Champions, kuwahamasisha hawa wanafunzi kufanya vizuri zaidi, maana tumegundua kuwa walipokuwa shuleni, tuzo za Uwezo ilikuwa ni chachu ya kuchukua hatua, lakini kwa sasa wanahitaji motisha wa aina nyingine kupiga hatua zaidi."

TANGAZO

HJFMRI

HJF Medical Research International, Inc. Tanzania

# EMPLOYMENT OPPORTUNITY

Join us in our efforts to end the HIV epidemic in Tanzania. Be part of the winning team to advance global health and save the lives of people living with HIV.

**About HJFMRI Tanzania Program**

The Walter Reed Program Tanzania (WRP-T) is a collaborative effort that supports PEPFAR-funded HIV prevention and treatment activities in the Southern Highlands and within the Tanzania People's Defense Forces (TPDF). HJF Medical Research International, Inc Tanzania (HJFMRI-T) is a local non-profit that has supported these efforts since 2004 for the Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR). PEPFAR activities are conducted in close collaboration with the Tanzania Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children; and the President's Office of the Regional Administration and Local Government (PORALG), through the Regional and Council Health Management Teams.

HJFMRI-T provides care and treatment to people affected by HIV/AIDS, and has been actively involved in HIV and AIDS programming, providing resources, personnel, and services to the Southern Highlands Zone. The program has expanded from supporting the Mbeya Zonal Referral Hospital to becoming a hub for anti-retroviral treatment in the zone; to community support through decentralized services, with the overall objective of implementing research, clinical HIV, prevention, care, and treatment services. HJFMRI-T currently focuses specifically on four regions in the Southern Highlands zone, namely Mbeya, Rukwa, Katavi, Songwe and Ruvuma for VMMC services only. The program also supports TPDF to implement comprehensive HIV prevention care and treatment program in 21 sites throughout the country.

**Employment opportunities:**

HJF Medical Research International, Inc. Tanzania (HJFMRI-T) is seeking qualified candidates to fill the positions listed below:

Cover letters and resumes should be sent by mail through post/EMS/DHL/ or any reliable Courier to the Human Resources and Administration Manager, P.O. Box 6396, Mbeya, or sent through e-mail to recruitment@wrp.or.tz. NOTE: To be considered, applicants must put the TITLE OF THE JOB in the SUBJECT LINE. "CVs should not include any reference to marital status, birthplace, or tribal or religious affiliations. Any CVs containing this information will not be considered for employment". Applications that are hand-delivered will not be accepted. The deadline for submitting the application is December 31, 2020. Those who do not meet the minimum requirements, as detailed in the job description below, will not be considered.

| | | |
|---|---|---|
| Job Title | : | Senior Training Manager |
| Reports to | : | Operations Director |
| Location | : | Mbeya |
| Duration | : | 12 Months (with an option to renew subject to availability of funds and need) |

**General overview**

As part of HJFMRI Tanzania we are seeking a Senior Training Manager who will be the point of contact for all technical and general training queries and training administration across WRP/HJFMRI Tanzania. We are looking for a professional Training Manager to ensure the smooth and effective functioning of training events and special projects. the Training Manager should be capable of providing support to the management; design, coordination, and conduct large and small-scale training activities will be conducted throughout the Southern Highlands. S/he will also be responsible for all training administration, scheduling, and coordination of training, while continually seeking to identify improvements to deliver training efficiencies and cost-effectiveness. This role is based in Mbeya, Tanzania, and will involve traveling to for fieldwork.

**Duties and Responsibilities**

- Update and expand the TRAINSMART database including entry of all training events, administer training records and the input of training qualifications in conjunction with the Head of Departments
- Liaise with training providers both internally and externally in relation to course coordination, facilitation including liaising with MOH and other stakeholders and be responsible for associated training administration such as training schedules, bookings, pre and post course work (where relevant), evaluation sheets, certificates etc.
- Record recommendations for training based on an annual needs analysis conducted with Line Managers, HR, and other relevant departments
- Design and apply assessment tools to measure training effectiveness, together with relevant Heads of Departments and the CQI department
- Track and report on training outcomes
- Provide feedback to training participants and management
- Evaluate and make recommendations on training material and methodology
- Coordinate with the Events Manager to ensure logistics for training activities are complete
- Establish and maintain relationships with external training suppliers
- Manage training budget and maintain in-house training facilities and equipment
- Continually evaluate procedures to monitor and analyze course effectiveness.
- Coordinate regular training review boards with managers, CQI department and internal training providers to ensure current and future learning needs are addressed; training provision is efficient and effective.
- Identify internal and external training programs to address competency gaps
- Partner with internal stakeholders regarding employee training needs
- Organize, develop or source training programs to meet specific training needs
- Inform employees about training options and map out training plans for individual employees
- Maintain employee training records
- Build and distribute an internal training prospectus covering what training is available, dates, and times employees and managers can access. Recommend ways to promote and improve communication of training opportunities across HJFMRI-T.
- Responsible for assisting the HR Department and the business with the facilitation of all -Training and following up with managers and individuals where required.

**Knowledge and Qualifications**

- A Bachelor's degree in a related field, a holder of MPH or/and MBA will be an added advantage.
- Knowledge of TRAINSMART will be an advantage.
- Five years' work experience in coordinating multiple training especially in HIV/AIDS programs
- Should have knowledge in adult instructional and learning theory and principles, instructional design, training methodologies, learning management systems, and competency assessment
- Previous experience of working within a similar training role and environment.
- Experience in database management.
- Excellent IT skills.
- Good communication and negotiation skills
- Tenacious with a 'can do' attitude
- Ability to work under pressure and meet deadlines.
- Confident presentation skills with the ability to translate health and technical data for communication to non-technical personnel

| | | |
|---|---|---|
| Job Title | : | Program Pharmacy Technical Advisor |
| Reports to | : | Associate Director, Clinical Services |
| Location | : | Mbeya |
| Duration | : | 12 Months (with an option to renew based on the availability of funding and need) |

**General overview**

The Program Pharmacy Technical Advisor (PPTA) is the technical lead personnel responsible for planning, implementing, and evaluating all supply chain activities for HJFMRI/WRP-T HIV/ AIDS programs. He or she works closely with the Associate Director of Clinical Services and the Logistic Management unit of the Ministry of Health Community Development Gender Elderly and Children (MoHCDGEC), Medical stores Department (MSD), local partners and stakeholders for the development and implementation of supply chain procedures in support to adequate medicine quantification, procurement, warehousing, inventory management, ordering/issuing, and distribution.

The PPTA provides technical leadership and direction for developing and implementing innovative strategies and activities to support the strengthening of supply management systems in the Southern Highland Zone. The PPTA will also work with other WRP Regional teams to develop and deploy appropriate logistics management information systems that support the planning and monitoring of supply chain operations. He or she supports supply chain capacity-building efforts and ensures that systems and processes are in place to assure the continuous availability of key program commodities. The PPTA ensures activities are based on the annual HJFMRI-approved Supply chain work plan. The full-time position is at HJFMRI/WRP Office in Mbeya, Tanzania, with 40% and 5% Domestic and Foreign travel, respectively, and reports to the Associate Director of Clinical Services.

**Duties and Responsibilities**

- Assist the Associate Director of Clinical Services in the development of Supply Chain work plans and budgets as they relate to supply chain activities. Provide input into updating and implementing the annual work plan and budget for PEPFAR supported Medicine for Opportunistic Infections.
- Provide technical assistance to WRP Regional teams and local partners to quantify HIV/AIDS products and other key commodities, including establishing appropriate forecasting and supply planning mechanism and information systems to assure the availability of data necessary for adequate quantification.
- Collaborate with the WRP Regional Teams and local partners to ensure that effective and efficient warehousing and distribution systems are in place for HIV/AIDS medicines and other key commodities.
- Participate in identifying and prioritizing capacity development activities to strengthen national and regional level pharmaceutical supply chains, and build expertise in monitoring and supervision in collaboration with WRP Regional Teams and other relevant team members and partners. Develop and implement appropriate training and supervision programs.
- Provide technical assistance to WRP-SC team and other treatment partners on OI medicine issues, including drug product quantification, procurement, and distribution.
- Represent the HJFMRI/WRP program at various technical meetings with other cooperating agencies, collaborating partners, senior government officials, and/or donor agencies in matters related to the supply chain.
- Provide technical assistance to assess current HIV/AIDS pharmaceutical management practices and develop action plans and recommendations to address priority issues to improve the related supply chain's effectiveness.
- Provide TA to develop standard operating procedures (SOPs) for inventory management and other aspects of supply chain management that will assure the availability and quality of medicines and other commodities.
- Provide supervision to other SCM team members and be held accountable for their performance management (including regular results, check-ins, formal appraisals, supportive supervision, rewards, training, coaching, and career development support).
- Monitor and document progress of activities toward achieving results of the supply chain activities of the approved HJFMRI/WRP-T work plan through periodic measurements of indicators.
- Participate in developing regular quarterly and semi-annual reports on the work plan for Supply chain activities for HJFMRI/WRP HI/AIDS program as needed. The PPTA is also expected to draft regular activity progress reports, closely monitor activities assigned to the Regional SC team to meet results and budget targets.

# TANGAZO

- Provide technical assistance to WRP Regional team and other treatment partners in the area of Pharmacovigilance.
- Produce any other ad hoc reports or updates on activities, as required or requested by Donors.
- Make regular presentations of results and progress to stakeholders. Participate and make representations on relevant program work in technical meetings as needed.
- Facilitate the work of external consultants as required.
- Undertake other relevant activities as requested by the Associate Director of Clinical Services
- Organizing and Coordinating Commodity and Performance review meetings in Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Songwe, and Katavi Regions.
- Assist the Regional teams in the development of Scope of works and budgeting of all activities related to supply chain, commodity management, and performance review meetings
- Organize for the necessary logistics involvement for teams to conduct the meetings.
- Liaise with Region Technical Coordinators to consolidate meeting resolutions (supply chain and commodity management) and share with teams of implementers
- In collaboration with Regional Technical Coordinators, R/CHMTs supervise implementations of all agreed resolutions (supply chain and commodity management) at the site level.
- Works with the various Departments Lab, M&E, Outreach, CQI, Contracts, and program teams (Advisors), for Identification and prioritization of Expectations and Core Essential activities for implementation by WRP Regional teams.

**Knowledge and Qualifications**

- A basic degree in pharmacy (Bachelor Pharmacy or it's equivalent) with the added advantage of Masters of Public Health
- Five years of post-training experience as a practicing pharmacist
- Three of these should be in direct HIV/AIDS service provision.
- Three years' experience in planning and budgeting pharmacy-related commodities
- Five years' experience in logistics management information system
- Understanding of MOHCDGEC structure and operating system
- Understanding the policies and practices of the Tanzania national commodity management system
- Basic understanding of the USG commodity management system
- Basic training and experience in adherence counseling are preferred.
- Leadership and management experience is preferred.
- Demonstrated ability to build and maintain relationships with senior colleagues, particularly interacting with government agencies, NGOs, the private sector, and donor agencies
- Good communication skills
- Proficiency in the use of the English language, both oral and written
- Basic computer skills, including use of software-based recording and reporting of pharmacy services

| | | |
|---|---|---|
| **Job Title** | : | **Senior Accountant** |
| **Reports to** | : | **Senior Manager, Accounting** |
| **Location** | : | **Mbeya** |
| **Duration** | : | **12 Months (with an option to renew based on the availability of funding and need)** |

**General Overview**

This position is responsible for day to day transactional accounting operations of HJFMRI-T operations. The Senior Accountant will serve as a point person for accounting and provide supervision, coaching, and support to program staff and any other junior accountant in the department. He / She is responsible for ensuring compliance with all applicable accounting policies and procedures, laws, and regulations requirements.

**Duties and Responsibilities**

- Provide leadership and supervision of other department accountants (s)
- Ensuring daily accounting activities are executed with the right ethical practices.
- Perform accounting activities to include financial reports, bank reconciliations, general ledger entries, and other general accounting functions.
- Ensure the document workflow's efficiency within the department from the point request is made, approval, final payment, and reconciliation.
- Maintain, monitor accounts, and finance helpdesk to ensure that issues raised by other staff are responded to and resolved timely.
- Maintain and reconcile petty cash accounts monthly to be reviewed by the accounting manager.
- Maintain robust financial reports in compliance with organizations' policies and procedures.
- Responsible for GL entries and accurate recordkeeping to support entries and transactions.
- Ensures timely monthly and annual accounting close.
- Resolves accounting issues, concerns, and questions on time to ensure smooth and efficient program operations and to report.
- Provides monthly accounting reports to finance and accounting staff for review.
- Assist in Payroll preparation monthly, payroll reconciliations, and resolving all payroll related issues.
- Reviews vs. prepare monthly reconciliations of all balance sheet accounts.
- Trains project accounting staff on HJFMRI procedures and policies.
- Assist with the preparation of financial reports for the US Government, institutional funders, and private donors as needed
- Respond to routine HQ accounting-related inquiries
- Provides support for internal and external audit support
- Review the completeness and accuracy of regional office and country office monthly, quarterly, and annual financial reports package submissions, resolve related problems and provide guidance to the country offices to resolve them appropriately.
- Maintain vendor files and related accounting records, such as leases and contracts
- Manage accounts payables, receivables, payroll, travel advances, and international wires
- Supports or leads on special projects as needed.
- Any other responsibilities as assigned by the accounting manager, in support of the team.

**Knowledge and Qualifications**

- Bachelor's degree in Accounting, Finance, Business Administration, or related field.
- ACCA/CPA (T) is an added advantage
- Five years minimum accounting and auditing experience, preferably in a nonprofit or international development environment
- Four years of supervision experience in mid to large accounting department
- Knowledge of and familiarity with accounting systems/packages
- Experience managing staff
- Ability to use good judgment and professionalism; experience in decision-making
- Excellent analytical skills
- Excellent Microsoft Excel skills and experience with QuickBooks accounting software
- Experience with US government regulations a plus
- Accuracy and attention to detail
- Ability to meet communicated schedules and deadlines
- Strong skills in internal controls and accounting standards
- Ability to function effectively both autonomously and on complex/sensitive issues and projects.
- High level of professionalism, transparency, and integrity in the overall production of work.
- Excellent written and oral communication skills in both English and Kiswahili
- Willingness to abide by all ethics and compliance policies of HJFMRI

| | | |
|---|---|---|
| **Position** | : | **General Accountant (2 Positions)** |
| **Reports to** | : | **Senior Accounting Manager** |
| **Location** | : | **Mbeya** |
| **Duration** | : | **12 Months (with an option to renew based on the availability of funding and need)** |

**General Overview**

HJFMRI-TZ seeks to hire a self-motivated and talented General Accountant. The purpose of this position is to ensure the accuracy of entries; timelines of payments and financial reporting to the program are done without delay. The position holder has to perform balance sheet reconciliations and provide advice and support to staff in financial management.

**Duties and Responsibilities**

- Prepare documents by scrutinizing and verifying that all required attachments have been supplied before documents are channeled for approval, posting, and payment process.
- Post entries into Quick Book daily.
- Ensure all entries posted into QuickBooks comply with the International Financial reporting standard, GAAP, and QuickBooks accounting and reporting manual.
- Initiating payments into the banking system or writing bank checks while ensuring segregation of duty is strictly for each paid document strictly observed between posting and payments.
- Ensure payments and all other processes comply with internal control policy and other policies.
- Prepare and submit all documents posted and paid through the bank to the senior accountants daily for QB check application and reconciliation purposes.
- Maintain the document workflow system and ensuring the document workflow template is fully updated with daily posting and payments made.
- Ensure all payments are correctly scanned and submitted to HQ.
- Reconcile financial discrepancies and errors as reported by collecting and analyzing account information.
- Answer accounting procedure questions by researching and interpreting accounting policies and regulations.
- Enforce internal policies to program staff, e.g., Training SOP, Travel advance policy, Mpesa policy, and other program policies.
RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inahitaji kuwapo shughuli za uwekezaji, ili kuharakisha kasi ya maendeleo na kukuza uchumi wa taifa.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi Ikulu jijini Zanzibar, alipokutana na ujumbe wa wawekezaji wa Kampuni ya Ozuaydin kutoka nchini Uturuki, ulioongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Mahmet Aydin, ambao umeonyesha nia ya kuwekeza katika ujenzi wa bandari, uwekaji wa vifaa pamoja na uendeshaji wa shughuli za bandari eneo la Malindi na Mpigaduri, sambamba na ujenzi wa ukumbi wa kimataifa wa mikutano.

Alisema serikali iko tayari kushirikiana na wawekezaji kwa kuhakikisha inaweka mazingira mazuri yanayovutia ili kufanikisha azma hiyo. Aliwataka wawekezaji hao kuwasiliana na mamlaka zinazosimamia uwekezaji nchini, ili kupata miongozo na taratibu za kisheria zinazohusiana na jambo hilo.

Naye Mkurugenzi Mkuu kutoka Kampuni ya Uzuaydin, Mahmet Aydin, alisema kampuni yake imedhamiria kutumia fursa za uwekezaji zilizopo nchini baada ya kuridhishwa na mazingira bora yaliopo.

Alisema amefurahishwa na mapokezi mazuri ya serikali aliyoyapata na kubainisha uwekezaji wanaolenga kuufanya utakuwa na tija na maslahi kwa wananchi wa Zanzibar pamoja na nchi za ukanda huo.

Wakati huo huo, Rais Dk. Mwinyi, alikutana na ujumbe kutoka nchini Oman na kubadilishana nao mawazo juu ya maendeleo ya kulifanyia matengenzo makubwa jengo la ajabu (Beit el Ajaib), liliopo Forodhani Zanzibar na changamoto zilizojitokeza.

Dk. Mwinyi, aliipongeza Serikali ya Oman kwa juhudi kubwa inazozichukua kulifanyia matengenezo jengo hilo, kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano (MOU).

Alisema hatua ya kulifanyia matengenezo jengo hilo, itasaidia kulirejesha katika hali yake ya asili, na kuendelea kutumika na kuimarisha utalii.

Waziri wa Mambo ya Kale wa Oman, Ibrahim Al Kharous, alimpongeza Rais Dk. Mwinyi, kwa kufuatilia kwa karibu matengenezo ya jengo hilo muhimu katika ustawi wa sekta ya utalii nchini.

Katika hatua nyingine, juzi Rais Dk. Mwinyi amevunja Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kutokana na kutoridhishwa na uendeshaji wa shirika hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:

**Dar es salaam – 0768 928 516.**

**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**

## TUNAHITAJI MAFUNDI

**TUNAHITAJI MAFUNDI WA PIKIPIKI WENYE UZOEFU, UMRI MIAKA 25-35.**

**TUMA MAOMBI KWA: linkallafrica@gmail.com**

**MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI: 17/12/2020.**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MEDEUS EDWARD MWASHA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI **MC 976 BET** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOKO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI ARU/ARU/RB/774096/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ESTERMANA LAZARO SWAI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye namba za usajili **T 130 BLU.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/MAG/RB/774197/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BAHAYE IBRAHIM** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0231-0011** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **SUMVE SEKONDARI October, 2006.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: MOR/MOR/RB/856257/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HAIKA ELIAWONY MONGI** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index **namba S.3068/0023** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **RASESA SEKONDARI** mwaka **2015.** Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0356/0508** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **VUNJO HIGH SCHOOL** mwaka **2018.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/GOG/RB/863419/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAINESS SILAS SELENDO** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0983/0003** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekonday TUMAINI LUTHERAN SEMMINARY mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/846112/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MEDEUS EDWARD MWASHA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI **MC 976 BET** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOKO KARIBU.

**TAARIFA YA POLISI ARU/ARU/RB/774096/2020**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**RUFAA/MADAI/JINAI NO. 45/2020**
**katika Mahakama ya Wilaya Dodoma**

**Shauri la Rufaa/Madai No.45/2020**
**katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma**
**PAUL STEVEN MUKOBA............Mrufani**
**Dhidi ya**
**1. MENEJA (HAZZEM SACCOS)............ Mrufaniwa**
**2. HILDA MKOBA**

Kwa: **HILDA MKOBA**
**DAR- ES- SALAAM.**

Kwa kuwa Rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya JUMATATU Tarehe 18/1/ Mwaka 2021 unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 11/12/2020.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**RUFAA/MADAI/JINAI NO. 46/2020**
**katika Mahakama ya Wilaya Dodoma**
**Shauri la Rufaa/Madai No.46/2020**
**katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma**

**PAUL STEVEN MUKOBA.........Mrufani**
**Dhidi ya**
**1. MENEJA (HAZZEM SACCOS).........Mrufaniwa**
**2. HILDA MKOBA**
**3. YONO ACTION MART**

Kwa: **HILDA MKOBA**
**DAR- ES- SALAAM.**

Kwa kuwa Rufaa iliyotajwa hapo juu itasikilizwa katika Mahakama iliyotajwa hapo juu siku ya JUMATATU Tarehe 18/1/ Mwaka 2021 unatakiwa uhudhurie katika Mahakama hiyo Mrufani/Mrufaniwa/Shahidi pamoja na vielelezo kama vipo.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Mhuri wa Mahakama hii leo 11/12/2020.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 194/2020**
**Ombi la IVAN O. NATHANIEL kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu JAISON P. MASANIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **05/01/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 15/12/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANNA JOSIAH OPIYO** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0214-0007** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MSALATO mwaka 1996, yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **UMB/RB/1220/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAFIDH SAID SHEIKHE** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **HONDA** yenye namba za usajili **T 148 CZT,** chasis namba **GN77A130797** engine namba **IME0732103**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **PWA/MLA/RB/845324/2020**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# Ujerumani yaongeza vizuizi kuelekea mwisho wa mwaka

**Born,** UJERUMANI

UJERUMANI imeongeza vizuizi ikiwamo kufunga shule na biashara ambazo sio muhimu katika kukabiliana na maambukizo ya Covid-19.

Hatua hiyo ni hadi Januari 10, mwakani, huku kipindi cha Krismasi kila ikiruhusiwa kuwa na wanafamilia isiyozidi watu wanne.

Nchi hiyo iliripoti vifo vingine 952 na visa 27,728 hadi siku ya Jumatano.

Nchi zingine za Ulaya zimeimarisha vizuizi kabla ya Krismasi na Ufaransa ikianzisha amri ya kutotoka nje wakati wa usiku.

Chini ya hatua hiyo nchini Ujerumani, biashara muhimu tu kama vile maduka makubwa na benki zitaruhusiwa kubaki wazi.

Migahawa, baa na vituo vya burudani vimefungwa tangu Novemba na maeneo mengine ya nchi yalikuwa yameweka vikwazo vyao wenyewe.

Pia saluni ni miongoni mwa biashara ambazo lazima zifungwe, wakati kunywa pombe, kama vile vibanda maarufu vya divai ni marufuku.

Kampuni zinahimizwa kuruhusu wafanyakazi kufanya kazi nyumbani. **BBC**

# Yaitaka Google kufunga vituo kadhaa vya YouTube

**Kampala,** UGANDA

TUME inayosimamia Mawasiliano Uganda (UCC) imeandika barua kwa kampuni ya Marekani ya Google, ikiitaka kampuni hiyo ifunge stesheni kadhaa za televisheni zinazopeperusha matangazo yake kupitia You tube.

Miongoni mwa stesheni hizo ni Ghetto TV, inayomilikiwa na Chama cha National Unity Platform (NUP) cha mgombea wa urais Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine.

UCC inataka karibu stesheni 13 zinazopeperusha matangazo yake moja kwa moja kupitia YouTube, kufungwa kwa msingi kwamba zimekiuka sheria na maadili ya habari nchini Uganda.

Barua ya UCC kwa Google inasema kwamba tume ya mawasiliano ya Uganda imepokea malalamiko kadhaa kutoka kwa maofisa wa serikali, akiwamo Waziri wa Mambo ya Ndani, mwenyekiti wa usalama wa taifa, polisi na jeshi la nchi hiyo, kuhusu habari zinazopeperushwa na vituo hivyo vinavyotumia YouTube.

Barua hiyo inaeleza kwamba vituo hivyo vinapeperusha habari ambazo zinavunja sheria ya mawasiliano ya Uganda, ya mwaka 2013 na sheria inayosimamia habari ya mwaka 2019, ibara ya 8 sehemu ya 2.

Televisheni ambazo zimetajwa kwenye barua ya UCC ni pamoja na TMO Online, Lumbuye Fred, Trending Channel Ug, Uganda Yaffe, Uganda News Updates, Ghetto TV, Busesa Media Updates.

Nyingine ni Uganda Empya, Map Mediya TV, KK TV, Ekyooto TV, Namungo Media, JB Muwonge na Bobi Wine 2021. Barua hiyo inadai kwamba televisheni hizo kwenye mtandao wa YouTube, zilitumika kueneza machafuko ya hivi karibuni nchini Uganda yaliyopelekea vifo vya watu kadhaa na uharibifu wa mali.

Inaendelea kusema kwamba zinatumika "kueneza habari za uongo, na maoni potofu kwa nia ya kupotosha jamii, zikiwa na lengo la kusababisha ghasia kwa misingi ya kikabila na kisiasa.

Barua hiyo inaongezea kwamba habari na maoni yanayopeperushwa na stesheni hizo "yana upendeleo, yanaonyesha miili ya watu waliokufa, waliojeruhiwa vibaya, ajali mbaya na zinaweza kusababisha wasiwasi mkubwa katika jamii."

UCC inasema kwamba televisheni hizo za mtandao wa Youtube, hazina leseni ya kupeperusha habari nchini Uganda.

Kulingana na ibara ya 27 ya sheria ya maudhui nchini Uganda, hakuna mtu anaruhusiwa kupeperusha habari bila ya kuwa na leseni ya tume ya mawasiliano ya nchi hiyo na anayefanya hivyo anaweza kuhukumiwa mwaka mmoja gerezani, kulipa faini au kulipa faini na kifungo cha mwaka mmoja gerezani.

Mapema mwaka huu, UCC, iliamuru watu wote wanaoandika maudhui kwenye mitandao ya kijamii kusajili kurasa zao la sivyo wachukuliwe hatua za kisheria. Agizo hilo hata hivyo linaripotiwa kutotiliwa maanani.

Hatua hiyo inajiri wakati tume ya uchaguzi nchini humo inataka wagombea wote kufanya kampeni kwa njia ya internet kutumia mitandao ya You tube, Facebook, Twitter na kadhalika pamoja na radio, televisheni, kutokana na janga la virusi vya Corona.

Stesheni ambazo UCC inataka zifungwe, zinaonyesha sana kampeni za wanasiasa wa upinzani. **VOA**


**GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED**

GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED GAMCL

Head Office: P.O.BOX 40855 Dar es Salaam - Pugu station Bangulo
Mob: + 255 714 635599/ + 255 785 636864/ + 255 756 753 884
Branch: Mkombozi Bank Agrrey Street - Kariakoo/ Mwanza Rufiji Street
Branch: Kilombero Ruaha Morogoro
Email:gadauauctionmart@gmail.com/gadauauctionmart@yahoo.com
hashimugadau@yahoo.com

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA NA NOTICE YA SIKU KUMI NA NNE (14) ZA KULIPA DENI LOTE.**

Kwa idhini tuliyopewa na **BANK YA FINCA Microfinance Bank** tutauza kwa mnada wa hadhara **DHAMANA MBALIMBALI ZA WADAIWA WA BANK HIYO.** Mnada utafanyika kuanzia tarehe **31/12/2020 HADI Ukomo** mahali zilipo dhamana kuanzia **saa 4:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni.**

**UFUATAO NI MCHANGANUO WA MAJINA YA WADAIWA, DHAMANA NA MAHALI ZILIPO:**

| Na. | JINA LA MTEJA | TAWI | DHAMANA INAYOUZA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|---|
| 1 | MARIA SAIMON CHAULA | MBEYA | KIWANJA KIPO MAENEO YA UYOLE NSALAGA MBEYA MANISIPAA. |
| 2 | SAIDI C CHAUREMBO | MBEYA | KIWANJA KIPO MAENEO YA MASYETO MBEYA DISTRICT |
| 3 | ESTER J KIMARO | MBEYA | KIWANJA KIPO MAENEO YA UTENGULE MBALIZI MBEYA DISTRICT |
| 4 | GEOFREY M MWANGOSI | MBEYA | KIWANJA KIPO MAENEO YA ISYESYE MBEYA MANISPAA |
| 5 | ELIAS K MWAKASEKELE | MBEYA | NYUMBA IPO MAENEO MANGAVETA MBEYA MANISPAA |
| 6 | WITO D MWANDUNGA | MBEYA | KIWANJA KIPO MBALIZI MBEYA DISTRICT NA KIWANJA KINGINE KIPO UYOLE MBEYA MJINI PAMOJA |
| 7 | VENANCE J MWAKYABALA | MBEYA | NYUMBA IPO VETA NA KALOBE MBEYA MANISPAA |
| 8 | BARAKA B MWAKISORE | MBEYA | KIWANJA KIPO ISYSYE MBEYA MANISPAA |
| 10 | FELIX ANDREA NJAU | SONGEA | KIWANJA KILICHOPO MKUZO B" KWENYE PLOT 3083 BLOCK 'S' SONGEA MJINI |
| 12 | JULIANA ROCK LIKUNGUALA | SONGEA | KIWANJA KILICHOPO MSHANGANO-NAMANYIGU KWENYE PLOT No.591 BLOCK 'A' SONGEA MJINI |
| 13 | PETER PETER MAPUNDA | SONGEA | KIWANJA KILICHOPO MTAA WA RUVUMA SONGEA MJINI |
| 14 | JABU MOHAMED ALLY | SONGEA | KIWANJA KILICHOPO MTAA WA RUVUMA SONGEA MJINI |
| 15 | HAMIS SALANJE CHUMA | SONGEA | KIWANJA KICHOPO MSHANGANO –NAMANYIGU SONGEA MJINI |
| 16 | OMBENI KYALUTA MKINGA | SONGEA | KIWANJA KILICHOPO LUHIRASEKO-SEED FARM SONGEA MJINI |
| 17 | GALUS JOPHEREY MBAWALA | SONGEA | NYUMBA ILIYOPO MSHANGANO SONGEA MJINI |
| 18 | GERALD JOSEPH NCHIMBI | SONGEA | KIWANJA KILICHOPO KWENYE PLOT 1853 BLOCK 'SS' MKUZO SONGEA MJINI |
| 19 | CHEKA O. MPETE | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO KAPOLO IFAKARA MJINI |
| 20 | GODFREY M. MWACHA | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO KIYONJO IFAKARA |
| 21 | JAMES M.SENGEREMA | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO KATINDUKA IFAKARA MJINI. |
| 22 | JUMA S. MVES | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO MANG'ULA WILAYANI KILOMBERO |
| 23 | NAFTALI M. YUSUF | IFAKARA | KIWANJA KILICHOPO KAPOLO IFAKARA MJINI |
| 24 | JOYCE W. MANYUKA | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO MANGWALE IFAKARA MJINI |
| 25 | ELIZABETI L.MPANGO | IFAKARA | KIWANJA KILICHOPO KAPOLO IFAKARA MJINI |
| 26 | TOMAS T.LIWONGWE | IFAKARA | KIWANJA KILICHOPO KATINDIUKA IFAKARA MJINI |
| 27 | ALFRED A. SHABOO | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO KAPOLO IFAKARA MJINI |
| 27 | TWAHA S. TEMA | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO MIANZINI MBASA IFAKARA MJINI TOWN. |
| 28 | RASHID R. NDOMONDO | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO MANG'ULA WILAYANI KILOMBERO |
| 29 | MOHAMED MICHAEL KITUNGULU | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO MTAA WA JONGO KWENYE PLOT NO. 289 BLOCK "F" IFAKARA MJINI , NYUMBA ILIYOPO KIBAONI KWENYE PLOT NO. 94 BLOCK M IFAKARA MJINI, |
| 30 | BENJAMINI MLALA.MASSEPO | IFAKARA | NYUMBA ILIYOPO KWA SHUNGU IFAKARA MJINI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa "kama zilivyo " as where is basis"
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hatimiliki, kutwaa nyumba/dhamana kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuonana kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**WOTE MNAKARIBISHWA**

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**GADAU AUCTION MART AND COMPANY L.T.D**
**S.L.P 40855, DAR ES SAALAM, SIMU; 0714 635599/ 0785 636864**



JCL JOSINA CO. LTD

**JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.**

**DALALI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA – MKOA WA MWANZA-BUKOBA, MUSOMA NA GEITA**
**DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING**
**HEAD OFFICE –Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza**
**P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040, josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com**

**TANGAZO-TANGAZO-TANGAZO**

**JOSINA COMPANY LIMITED ITAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KUANZIA TAREHE 31/12/2020 NA MUDA NI KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA. KWA IDHINI/MAMLAKA TULIYOPEWA NA FINCA MICROFINANCE BANK.**

| | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|
| 1 | MARTIN ISSAYA TRIPHON | NYUMBA | KASHURA |
| 2 | MALIUS R KAWAMALA | NYUMBA | HAMGENDE |
| 3 | LAMECK N ORINDA | NYUMBA | IGABILO |
| 4 | SPERATUS SOSPETER NGAIZE | NYUMBA | NYAKANYASI |
| 5 | JACKSON K METHEW | NYUMBA | KARAGWE |
| 6 | KHARIDI GALIATANO | NYUMBA | MIGELA |
| 7 | RAMADHAN NURU SHABANI | NYUMBA | NYAKANYASI |
| 8 | KALUGILA MATIAS MWEHONGE | NYUMBA | KAHOLOLO |
| 9 | BARIKI ELIAS MUSH | NYUMBA NO 55364 PLOT NO 85&87 BLOCK "D" | KARAGWE |
| 10 | WISTON R KAMWONA | SHAMBA, KIWANJANA NYUMBA | KISINDI |
| 11 | PROFESTUS MTUI | NYUMBA | BURUMBA |
| 12 | JAFARY B SALEHE | NYUMBA | KEMONDO |
| 13 | KAMGISHA WISTON WILLSON | NYUMBA | KAGONDO |
| 14 | MUSTAFA NASSORO RASAWA | NYUMBA | BUYEKELE |
| 15 | ANTIDIUS KAIZILEGE | NYUMBA | RWAMISHENYE |
| 16 | HAKIMU ABDALA TORITOIJWA | NYUMBA | KASARANI/CUSTOM |
| 17 | GILBERT GOSBERT KAMARA | NYUMBA | OMURUSHAKA-KARAGWE |
| 18 | SYLIAKUS ELIAS KAJUMLO | SHAMBA NA KIWANJA | BUKOBA MJINI |
| 19 | ROBERT R RWEYENDERA | NYUMBA | KAYANGA - KARAGWE |
| 20 | NGUTU M NGAYE | NYUMBA | IGABILO – BUKOBA VIJIJINI |
| 21 | WINFRIDA K MUJONO | KIWANJA | INSHAMBYA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. DHAMANA ZITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA.75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI ZA UMILIKI ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
3. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA SIKU MOJA KABLA YA MNADA NA GHARAMA ZA KUMPELEKA MTEJA KWENYE DHAMANA ZITAKUWA JUU YA MTEJA.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA: -**
**MKURUGENZI Josina Co. Ltd: 0768 203 040, WHATSAPP NO: 0713 203 040.**

HABARI MICHEZO

# DEPAY AIKATAA BARCA, PSG




**LYON,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Lyon, Memphis Depay anachofikiria kwa sasa ni kushinda mataji na timu yake, licha ya kuhusishwa na Barcelona na Paris Saint-Germain.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 26 mkataba wake wa sasa na Lyon unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa sana na Barca ambayo inanolewa na kocha wa zamani wa Uholanzi, Ronald Koeman.

Amefunga mabao sita katika mechi 14 za Ligue 1 msimu huu, na kwa mujibu wa jarida la Ufaransa la Le Parisien, PSG wanamtaka Mholanzi huyo kucheza pamoja na Neymar na Kylian Mbappe mwakani.

Depay hivi karibuni alifunguka na kusema yupo tayari kuungana na Koeman pale Camp Nou, lakini alipoulizwa Jumanne na waandishi wa habari, alijibu tofauti kabisa.

"Nikiwa mkweli, tuna timu imara hapa," alisema. "Sijui nini kitatokea mwakani. Mimi ni mchezaji wa Lyon, nahodha, na nipo hapa kushinda vitu, mechi na kuwa muhimu.

"Hilo ndio dhumuni langu kubwa. Kama nikianza kufikiria kuhusu majaliwa yangu, naweza kupoteza umakini wangu.

"Kwa asilimia 100 mimi nipo Lyon. Nini kitakachotokea siku za usoni ni suala la kusubiri kwa sasa kuona."

# Ozil haondoki Arsenal Januari - Wakala

**LONDON,** England

WAKALA wa Mesut Ozil amebainisha kiungo huyo hataondoka Arsenal wakati wa dirisha la Januari, mwakani na kusisitiza mteja wake ana nia kubwa ya kumalizia kipindi cha mkataba wake kilichobaki.

Ozil aliondolewa kwenye kikosi cha Ligi Kuu England na Ligi ya Europa na Mikel Arteta Oktoba, mwaka huu na hawezi kuchaguliwa kwenye timu hadi wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari ambapo orodha inaweza kubadilishwa.

Kiungo huyo wa zamani wa Real Madrid, ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo wakati alipojiunga kwa ada ya pauni milioni 42 mwaka 2013, hajaichezea timu hiyo tangu Machi 7, mwaka huu.

Wakati wakala wa Ozil, Dk. Erkut Sogut, akisisitiza kuna klabu nyingi Ulaya zinamwania nyota huyo, amesema nyota huyo wa zamani wa Ujerumani ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu, anataka kumalizia mkataba wake Arsenal.

"Hata siku moja ni ndefu sana kwenye soka, kamwe huwezi kujua," alisema akiiambia Tuttomercatoweb.

"Bila shaka, kuna klabu nyingi zinamtaka kumsajili yeye, lakini anataka kwanza kumalizika mkataba wake.

"Hakuna kitu kilichobadilika katika uamuzi wake wa kutaka kwanza kumaliza mkataba wake na kutocheza kwake hakujabadilisha kitu."






# *PSG wajiandaa kutangaza kumsajili Messi*

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain inajiandaa kutangaza kumsajili Lionel Messi, kwa mujibu wa FootballTransfers.

Klabu hiyo ya Paris Saint-Germain kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumwania Messi mwenye umri wa miaka 33.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti za usajili, PSG inajiamini kwamba itamsajili nyota huyo wa Barcelona.

Messi, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, alijaribu kuondoka Barcelona mwishoni mwa msimu wa 2020-21, lakini mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or aliamua kubakia Camp Nou.

Sasa mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG wamejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili Messi kwa uhamisho huru.

Miamba hao wa jiji la Paris wameripotiwa kuanza mazungumzo binafsi na wawakilishi wa mchezaji huyo na kwamba wana uhakika wa kumsajili kipindi cha majira ya joto kijacho.

Hata hivyo, gazeti la Daily Star, limedai kwamba, Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola naye yupo kwenye mbio za kuwania kumsajili Messi.

HABARI MICHEZO

# Koeman atuma salamu PSG

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, ametuma ujumbe kwa mabingwa wa soka nchini Ufaransa, Paris Saint-Germain kwa kusema hawawaogopi.

Barcelona wamepangwa kukutana na PSG kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16, huku mchezo wa kwanza ukitarajiwa kuchezwa Camp Nou Februari 16, mwakani na mchezo wa marudiano kupigwa jijini Paris, Ufaransa, Machi 10, mwakani.

Koeman amesema wameipokea kwa mikono miwili ratiba ya hatua hiyo, na anaamini mpambano utakuwa na vuta ni kuvute, kutokana na wapinzani wao kuwa na wachezaji wenye viwango vya hali ya juu.

Amesema wanaiheshimu PSG kama mshindani wao, na hawatabweteka kwa kuamini historia ya michuano ya Ulaya imekua ikiwabeba mara kwa mara, licha ya msimu uliopita kukabiliwa na changamoto ya kuondoshwa kwa kipigo cha aibu na Bayern Munich.

"PSG ni timu yenye nguvu, lakini ni ngumu kwao kwa sababu sisi pia ni timu ngumu na naona ni sawa kabisa," alisema akinukuliwa na AS.

"Katika miaka ya hivi karibuni wametumia fedha nyingi kuijenga timu ambayo inaweza kupigania mataji makubwa kama Ligi ya Mabingwa.

"Msimu uliopita walifika fainali, na ni timu ambayo itaendelea kuwapo," amesema.

Msimu uliopita PSG walifikia hatua ya fainali ya michuano hiyo, lakini walifungwa na Bayern Munich waliobeba taji hilo.



# GUARDIOLA ALALAMIKIA UBUTU



**MANCHESTER,** England

KOCHA Mkuu wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema tatizo kubwa lililopo kwenye timu yake kwa sasa ni ubutu wa washambuliaji wake kushindwa kufunga jambo ambalo linahitaji muda kutafutiwa dawa.

Kocha huyo ameongeza kuwa walikuwa na nafasi ya kuibuka na ushindi kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu England dhidi ya West Brom, juzi Jumanne usiku, lakini wakalazimishwa sare.

City wakicheza kwenye dimba lao la Etihad ililazimisha sare ya kufungana bao 1-1 na West Brom na kuwafanya wagawane pointi moja moja inayowafanya City wafikishe pointi 20, wakiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Likay Gundogan alipachika bao la kwanza kwa City dakika ya 30 na dakika ya 43 Ruben Dias alijifunga na kuwafanya waende mapumziko wakiwa wametoshana nguvu.

Hadi dakika ya 90 zinakamilika timu zote ziligawana pointi na kuifanya West Brom kufikisha pointi 7 ikiwa nafasi ya 19.

Guardiola amesema walimiliki mchezo katika kila kitu ila walishindwa kutumia nafasi ambazo walizipata kipindi cha kwanza na kipindi cha pili, jambo lililowafanya washindwe kupata ushindi.

# *Lampard adai uchovu umeigharimu Chelsea*

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesema wachezaji wake wana uchovu kufuatia kukutana na kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Wolves katika mtanange wa Ligi Kuu England, uliochezwa juzi Jumanne.

Bao la Pedro Neto dakika ya 95 liliinyima Chelsea kuondoka na pointi moja pale kwenye dimba la dimbani Molineux.

Daniel Podence alisawazisha bao la mshambuliaji wa Ufaransa, Olivier Giroud ambaye aliitanguliza mbele The Blues.

Hicho kinakuwa kipigo cha pili mfululizo kwa Chelsea baada ya mechi ya juzi dhidi ya Everton kupoteza kwa 1-0.

Baada ya mchezo huo, Lampard alisema uchovu umewagharimu kwani walijipanga kwa ushindi.

"Nimekasirishwa na hili kwa kweli, tulistahili kupata ushindi, lakini mambo yalikuwa tofauti kabisa," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Naweza kusema uchovu wa wachezaji, lakini hiyo sio sababu kubwa, kikubwa tunatakiwa kujipanga kwa ajili ya mechi zijazo."

Wolves ipo nafasi ya 10 ikiwa na pointi 20, huku Chelsea ikiwa nafasi ya tano na pointi 22, zote zikiwa zimecheza mechi 13.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA NI STRAIKA BORA DUNIANI – ZIDANE

## Afunguka nyota huyo amekuwa akisaidia kuamua matokeo hata kwenye mechi...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amemsifia, Karim Benzema baaada ya mshambuliaji huyo kuisaidia Real Madrid kuifunga Athletic Bilbao kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumanne.

**Benzema alifunga mabao mawili ya dakika za majeruhi wakati Madrid wakiifunga Athletic 3-1 na kufikisha pointi sawa na Real Sociedad na Atletico iliyoko kileleni mwa msimamo.**

Mfaransa huyo alifikisha mabao 10 aliyofunga kwenye mashindano yote msimu huu, mengi zaidi kuliko mchezaji yoyote wa LaLiga.

Zidane alimsifia straika huyo, akisema uwezo wa Benzema ni mkubwa hata kwenye mechi inayoonekana kuwa ngumu kwao.

"Kwa upande wangu yeye ni bora kwa sababu pamoja na mchezo kuwa mgumu dhidi ya Athletic alifunga mabao mawili," alisema kocha huyo wa Madrid akiwaambia waandishi wa habari.

"Mara zote anakuwa fiti. Kuna wachezaji wakubwa wenye uwezo wa kuamua matokeo wakati wowote."

Toni Kroos alianza kuipa Madrid uongozi pale kwenye dimba la Alfredo Di Stefano, ambapo Athletic walicheza pungufu wakiwa na wachezaji 10 kuanzia dakika ya 13 baada ya Raul Garcia kuonyeshwa kadi nyekundu.

Lakini Ander Capa akasawazisha na Madrid wakajikuta kwenye wakati mgumu kabla ya Benzema kuwarudisha mchezoni.

Benzema amehusika katika mabao 18 kwenye mechi 22 za LaLiga dhidi ya Athletic, akifunga 13 na kutoa pasi za mwisho tano.

Zidane alikubali kwamba Madrid walianza kwa kucheza chini ya kiwango, na wapinzani wao walicheza kwa kujihami zaidi baada ya kubakia 10 uwanjani.

"Ni kweli kwamba, tulipata wakati mgumu. Unapocheza dhidi ya wachezaji 10, kama ukiwakamata vizuri unaweza kuwa mchezo rahisi zaidi kwako."

## ZISIKUPITE

### MESSI AKARIBIA PSG

MATUMAINI ya Paris St-Germain na Manchester City kumsajili Lionel Messi yamefufuliwa upya, baada ya mgombea urais wa Barcelona, Emili Rousaud kusema "ni vigumu kumudu" mshahara wa raia huyo wa Argentina mara mkataba wake wa sasa utakapomalizika msimu ujao. ***(AS)***

### ZABALETA AMFUNDA MESSI

MLINZI wa zamani wa Manchester City, Pablo Zabaleta amesema klabu hiyo ya Ligi Kuu England ni "mahali pazuri" kwa Lionel Messi ikiwa mchezaji huyo ataamua kuondoka Barca. ***(Stadium Astro, via Sun)***

### MBAPPE NJIA NYEUPE

KUNA "uwezekano mkubwa" Lionel Messi ataondoka Barcelona na kujiunga na PSG msimu ujao, huku mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 21, akitarajiwa kujiunga na Real Madrid. ***(TalkSport)***

### DEPAY NJIA PANDA

NYOTA aliyekuwa anawindwa na Barcelona, Memphis Depay (26), bado hajafanya uamuzi wa kuhusu hatima yake, huku nyota huyo wa Uholanzi akitarajia kumaliza mkataba wake ifikapo majira ya joto mwakani. ***(Goal)***

### MUSIALA MAMBO SAFI

BAYERN Munich ipo tayari kumpatia kiungo mshambuliaji wa kati, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 17, mkataba mpya ambao utamfanya kupata mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki licha nyota huyo kunyatiwa na klabu za Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### OZIL KUBAKIA ARSENAL

WAKALA wa Mesut Ozil amesema kiungo huyo wa kati wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 32, anataka kusalia Arsenal kukamilisha miezi sita ya mwisho ya mkataba wake - licha ya klabu hiyo kumtaka aondoke ifikapo Januari, mwakani. ***(Tuttomercato)***

### PSG, AOUAR KUTETA

PARIS St-Germain wako tayari kujadili mkataba wa winga wa Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, ambaye alikuwa akinyatiwa na Arsenal msimu uliopita. ***(RMC Sport, via Sun)***

### VIEIRA AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Arsenal na Marseille zipo kwenye mbio moja kuwania kumsajili kiungo wa Ureno, Fabio Vieira mwenye umri wa miaka 20 kutoka Porto. ***(Record)***

### LEEDA YAMTAKA TOMORI

KLABU ya Leeds United inamfuatilia mlinzi wa Chelsea na England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 22, kwa lengo la kumsajili wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. ***(Football Insider)***

### MOURINHO AMTAKA WINKS

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amesema kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Harry Winks (24), hataruhusiwa kujiunga na klabu nyingine kwa mkopo ifikapo Januari, mwakani. ***(Mirror)***

# HITIMANA AKARIBIA KUTUA MTIBWA SUGAR

Na Saada Akida

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, anatajwa yuko katika mazungumzo ya kujiunga na Mtibwa Sugar ya Manungu, Turiani mkoani Morogoro ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

**Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Hitimana alisema mazungumzo na mabosi wa Mtibwa Sugar yanaelekea ukingoni na endapo watakubaliana, atasaini mkataba wa mwaka mmoja.**

Hitimana alisema hatua ambayo walifikia hadi jana mchana ilikuwa nzuri na kilichobakia ni uhakiki wa mwisho wa mkataba huo.

"Bado sijasaini mkataba, ila muda huu (jana asubuhi), niko kwenye ofisi za Mtibwa Sugar kwa ajili ya mazungumzo ya mwisho na viongozi wao na kama tutaenda sawa, nitasaini mkataba ambao makubaliano yetu ni mwaka mmoja," alisema Hitimana.

Kocha huyo alisema ana imani mambo yataenda vizuri kwa sababu mazungumzo ya awali yalienda sawa ikiwamo suala la maslahi ambayo atayapata baada ya kukubali kuiongoza timu hiyo.

"Kama nitasaini, tumekubaliana nitaendelea kubaki na msaidizi ambaye alikuwa na timu hiyo kwa kuangalia upungufu wetu hasa kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo, tutajipanga kwa pamoja kuongeza nguvu kwa ajili ya kuimarisha kikosi," alisema Hitimana.

Naye Mkuregezi wa Bodi ya Mtibwa Sugar, Jamal Bayser, alisema tayari wameshapata kocha mpya watakayefanya naye kazi baada ya kupitia orodha ya majina mbalimbali ya makocha ambao walituma maombi ya kutaka kuifundisha timu hiyo.

"Ni mapema kutaja jina, tusubiri muda utakapofika tutaweka wazi, ila msimamo wetu msimu huu kutafuta kocha wa kigeni, nani ni baada ya kila kitu kwenda sawa," alisema Bayser.

Baada ya kujiuzulu kwa Zuberi Katwila ambaye sasa anaiongoza Ihefu FC, Mtibwa Sugar ilikuwa chini ya Kocha Msaidizi, Vincent Barnaba.




Kiungo wa Azam FC, Richard Djodi (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

## Dar24, La Liga wafanya tamasha

Na Mwandishi Wetu

CHOMBO cha Habari cha Mtandaoni cha Dar24 Media kwa kushirikiana na wasimamizi wa Ligi Kuu Hispania maarufu La Liga wamefanya tamasha la mpira wa miguu kwa kuzishindanisha timu nane bora za mitaa ya hapa jijini Dar es Salaam.

Lengo la tamasha hilo lililofanyika Jumapili iliyopita lilikuwa ni kuhamasisha vijana kuepuka matumizi na biashara ya dawa za kulevya, kupitia kampeni ya 'Shtuka'.

Kitanki FC waliibuka washindi wa shindano hilo baada ya kuifunga Palianda FC bao 1-0, kwenye mchezo wa fainali, na kujinyakulia zawadi ya vifaa mbalimbali vya michezo kutoka makao makuu ya La Liga, Uhispania. Mlinda mlango wa Palianda FC, Athuman Bonge, alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa mashindano hayo na kupewa zawadi kutoka DSTV.

Mwakilishi wa Dar24 Media, Shaban Kondo alisema lengo la kuandaa tamasha hilo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kuibua vipaji kama sehemu ya ajira kwa vijana.

Naye Mwakilishi wa La Liga nchini, Alvaro Paya, amesema uongozi wa ligi hiyo uliona juhudi za Serikali ya Tanzania pamoja na jitihada binafsi za Dar24 katika kuhamasisha michezo na kubadili maisha ya vijana kama ni nia sahihi na ya La Liga katika kuhamasisha mchezo wa soka duniani.

## Namungo haitaki mchezo kimataifa

Na Saada Akida

BAADA ya kulazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi usiku, kikosi cha Namungo kimeelekea Zanzibar kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na mchezo wake wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya El Hilal Obeida kutoka Sudan.

Namungo itawakaribisha Wasudan hao katika mchezo wa hatua ya kwanza utakaochezwa Desemba 23, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Namungo, Hemedi Morocco, alisema wanaenda kujipanga kwa ajili ya mechi yao hiyo ambayo maandalizi ya michuano hiyo ni tofauti na wanavyojianda na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Morocco alisema baada ya kufanikiwa kupata pointi moja dhidi ya Azam FC, na kuona mapungufu ya kikosi chake katika safu ya ulinzi baada ya beki wake, Edward Manyama kupata majeraha katika mechi hiyo.

"Awali tulikuwa na changamoto katika safu ya ushambuliaji, nimelifanyia kazi na naona mabadiliko kwa kutumia nafasi hizo vizuri, kuelekea michuano ya kimataifa tunahitaji kuwa makini kulingana na wapinzani wetu," alisema Morocco.

Aliongeza amewaangalia wapinzani wake kupitia video na hivyo anakiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kuwakabili na hatimaye kupata matokeo mazuri.

## Matukio awataka wasanii kubadilika

Na Sabato Kasika

MSHINDI wa mashindano ya Mr University mwaka 2002, Matukio Chuma amewataka wasanii nchini kuacha kuishi 'maisha ya bandia' na badala yake waonyeshe uhalisia wa maisha yao yalivyo ili jamii ijifunze kutoka kwao.

Matukio alitoa nasaha hizo jijini, Dar es Salaam jana, wakati akizindua kitabu chake kiitwacho Matukio ambacho kimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza chenye ujumbe usemao 'Nimejifunza naendelea kujifunza'.

Alisema vijana wanatakiwa kujitambua, kujijua na kutumia karama na vipaji vyao, lakini wakiwekeza katika ufahamu ili waweze kujiletea maendeleo.

"Ninasikitika kusema baadhi ya wasanii nchini wanatumia mitandao ya kijamii vibaya kwa kupiga picha hata magari ya gharama kubwa, ili waonekane wana kitu na kumbe sivyo," alisema Matukio.

Alisema ameamua kuandika kitabu hicho kinachoelezea historia yake na mafunzo kwa vijana, ili kwamba hata kama hatakuwapo duniani, basi ujumbe wake uendelee kusomwa na kuwapa mabadiliko vijana.

Michezo
Alhamisi Desemba 17, 2020
Nipashe



Benzema straika bora duniani – Zidane UKURASA 22



Golikipa wa West Brom, Sam Johnstone, akiokoa shuti lililopigwa na mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling (kulia), katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad juzi usiku. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Kaze atamba kikosi Yanga SC kimeiva

## ●●● Kocha huyo aeleza safu yake ya ushambuliaji sasa ni mwendo wa dozi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI timu yake ikiwa inaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema safu yake ya ushambuliaji imekuwa na mabadiliko na inampa matumaini ya kuendelea kufanya vyema kwenye ligi hiyo inayoendelea hapa nchini.

**Kaze alisema hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Singida United iliyochezwa juzi.**

Kocha huyo raia wa Burundi alisema sasa hivi kikosi chake kimeanza 'kuvuna' idadi kubwa ya mabao tofauti na alivyoikuta timu hali ambayo inamwongezea nguvu kwenye mapambano yake.

Alisema mechi mbili walizocheza ikiwamo dhidi ya Mwadui FC ambayo walishinda mabao 5-0, ameona jinsi washambuliaji wake walivyokuwa makini kutumia nafasi za walizotengeneza.

Alisema uko utofauti mkubwa kwenye safu ya ushambuliaji ya awali na sasa ambayo imezidi kuimarika na kupata matumaini ya kushinda idadi ya mabao mengi katika mechi zao zinazofuata.

"Tukirudi katika mechi za nyuma tumekuwa tunashinda bao 1-0, 2-1 na kutokuwa makini na utulivu wa kumalizia nafasi za mwisho, sasa nimeona tofauti kubwa kupata imani kwamba tutafanya vizuri zaidi ikiwamo suala la kufunga idadi kubwa ya mabao," alisema Kaze.

Kuhusu kiwango kilichoonyeshwa na mshambuliaji wake mpya, Saido Ntibazonkiza, alisema hana wasiwasi na nyota huyo ambaye akishirikiana vyema na wachezaji wenzake watafikia malengo yanayotarajiwa na klabu hiyo.

"Nafahamu uwezo wa Saido, ni mzuri na amecheza soka kwa muda mrefu, kwa uzoefu wake kwa kushirikiana na nyota ambao amewakuta hapa tutafanya vizuri na kufunga idadi kubwa ya mabao katika mechi zetu zijazo za ligi na hata michuano mingine iliyopo mbele yetu," alisema Kaze.

Aliongeza kutokana na kiwango alichokionyesha mshambuliaji huyo, anafikiria kumjumuisha katika mipango yake kuwakabili Dodoma Jiji FC, mchezo utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha.

Mbali na kufunga mabao mawili, moja likiwa na mkwaju wa penalti, lakini kiungo huyo alionekana mbunifu kwa kutoa pasi nyingi za mwisho, akiwa kwenye eneo la hatari, lakini washambuliaji waliocheza mechi hiyo, Waziri Junior na Ditram Nchimbi, walishindwa kuzitumia nafasi hizo.

"Nimeona watu wamefurahi, na hii ni mechi yangu kwa kwanza, na Mungu akipenda nitafanya vizuri zaidi ya hii," alisema mshambuliaji huyo.

Kuhusu Ligi Kuu Tanzania Bara, Saido alisema hajacheza hata mechi moja, hivyo hawezi kusema kama ni ngumu au la, lakini anachojua zaidi kuna mechi moja tu ambayo ni ngumu zaidi, lakini atapambana.

Katika mechi hiyo ya kirafiki, Saido alifunga mabao mawili na la tatu liliwekwa kimiani na Deus Kaseke dakika ya 81.

Baada ya mechi hiyo, vinara hao wa Ligi Kuu Bara watasafiri kuelekea Mbeya kuwafuata wenyeji wao Ihefu FC katika mchezo utakaofanyika Desemba 26, mwaka huu na siku tano baadaye watavaana na Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga.

## Bocco: Tutawashika

**Na Somoe Ng'itu**

NAHODHA wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, John Bocco, amesema kikosi chake kitaendelea kupambana katika kila mechi wanayocheza hadi mwisho wa msimu na wanaamini nafasi ya kutetea ubingwa bado wanayo.

Bocco aliliambia gazeti hili kila siku kikosi chake kinaimarika kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri, ili wajiweke kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Mshambuliaji huyo alisema wanafahamu ushindani umeongezeka zaidi na hali hiyo inawaongezea hamasa ya kujituma kwa sababu wapinzani wao pia wanayataka mafanikio.

"Kila siku tunaimarika, tunajiimarisha kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri, kila timu inahitaji ubingwa, lakini sisi tunauhitaji zaidi kwa sababu uko mikononi mwetu," Bocco alisema. Aliongeza mbali na Ligi Kuu Tanzania Bara, mazoezi na maandalizi wanayofanya kila siku yanazingatia jukumu la kupeperusha bendera ya nchi ambalo wanalo.

Nyota huyo anayeongoza katika kupachika mabao alisema kwake anajipanga kujituma na kucheza katika kiwango bora kila atakapopata nafasi na anaamini kwa kufanya hivyo ataiweka timu yake kwenye nafasi nzuri.

Simba sasa inajiandaa na safari ya kuelekea Zimbabwe kwa ajili ya mechi yake ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum itakayochezwa kati ya Desemba 22 na 23, mwaka huu jijini, Harare nchini humo.

Wawakilishi hao wa Tanzania Bara katika michuano hiyo ya kimataifa wakirejea nchini wataendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwakabili Azam FC katika mchezo utakaofanyika Desemba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam na Desemba 30, mwaka huu itawafuata Dodoma Jiji FC kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042